Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

# Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 79 No. 201 | JAM. I-JAM. II 1439 AH | FEBRUARI 2019 | TABLIGH 1398 HS | BEI TSH. 500/=

**Nukuu ya Qur'an Tukufu**

Na katika watu wako wanaoshikawashirika kinyume cha Allah, wanawapenda kama kumpenda Allah. Wakati wale walioamini wanampenda Allah zaidi (kuliko vitu vyote);.....
(Al- Baqara 2:166).

# Tafuteni Radhi ya Allah

## • Omba Msamaha • Tumia Ndimi kwa Upole • Onesha Mabadiliko Mema

Na Mwandishi Wetu

Katika hotuba ya tarehe 4/01/2019, Baada ya Tashahhud,Taawwudh na Surat Faatihah, Kiongozi wa Jumuiya Ahmadiyya duniani, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] alisema:

Leo ni Ijumaa ya kwanza ya mwaka wa 2019. Kuhusiana na jambo hili mimi kwanza napenda niwatakie heri ya mwaka mpya Waahmadiyya duniani kote, Allah aufanye mwaka huu uwe wenye baraka, na ulete kila aina ya mafanikio. Lakini sisi tunatakiwa kukumbuka jambo hili kwamba hakuna faida katika kutakiana heri sawa na kawaida inayotumika. Na wala kawaida ya kutakiana heri ya aina hii haitusaidii kupata radhi ya Allah. Hakika ya kupata Baraka za kweli za Allah za mwaka mpya ni hii kuwa sisi tufanye ahadi ya kwamba Allah Aliyetujaalia kuona jua lingine la mwaka mpya, ametuingiza humo, nasi tunatakiwa kujitahidi kuondoa udhaifu, na giza lililo ndani yetu. Yaani yale mapungufu na makosa tuliyoyafanya mwaka jana tufanye ahadi ya kuyaondoa. Tujitahidi kuonesha mabadiliko mema ndani yetu zaidi kuliko mwanzo ambayo tulifanya ahadi ya baiati kwa Masihi Aliyeahidiwa[as] kwa ajili yake. Masihi Aliyeahidiwa[as] akielezea hali ya Muahmadiyya inatakiwa iweje anasema katika sehemu moja; "Mtu hatakiwi kuamini jambo hili tu baada ya kujaza baiati kuwa Jumuiya ni ya kweli, na kwamba kwa kuamini hivyo yeye anapata Baraka," amesema kuwa "... baada kuingia kwenu katika Jama'at mnatakiwa kujitahidi kuwa watu wema, wacha mungu, na mnaojiepusha na kila aina ya ubaya... usiku na mchana mbakie katika unyenyekevu wa hali ya juu... mnaotumia ndimi zenu kwa upole, kuomba msamaha kuwe ni kitendo chenu cha kudumu, muombe dua katika sala zenu," dua zitakuwepo katika

*Endelea uk 5*



*Hadhrat Khalifatul Masih V a.t.b.a. akihutubia Ijumaa katika msikiti wa Baitul Futuh uliopo jijini London nchini Uingereza ambapo hotuba yake hurushwa mubashara kupitia satelaiti duniani kote kupitia MTA.*

# Lengo la Dini Sio Siasa au Kuwa na Dola



Na **Musa S. Mgeleka**

*Hakuna karaha katika dini; hakika uongofu umekwisha pambanuka katika upotevu; basi anayemkataa shetani na kumwamini Allah, bila shaka yeye ameshika kishikio kigumu kisichovunjika; na Allah ni asikiaye, ajuaye.* (2:257)

Lengo la siasa au dola ni kukamata dola kwa gharama yoyote iwayo. Ulinzi wa dola ni kwa sheria zake, viongozi wake na watu wake na mali zao na mipaka yake. Dola hugharamia majeshi kulinda hayo na yeyote atakayevunja sheria za nchi yake, kuwadhuru viongozi na watu wake na mali zao na kuvuka mipaka ya nchi hupambana na nguvu ya dola. Ama atateswa, kufungwa na au kuuawa.

Asili ya dini zote ni Islamu na asili ya dini hizi ni moja. Kwenye dini sheria za dini, viongozi na watu wake na mipaka ya dini, mwanadamu hana mamlaka ya moja kwa moja kuvilinda bila kwanza ruhusa ya Allah maana mlinzi wa dini ni Allah. Kwenye dola majeshi yamepewa mamlaka ya moja kwa moja kuilinda dola. Ikiwa mkuu wa nchi akiwa mlinzi mkuu.

Mwenye dini hata mateso yapatikane makubwa ya namna gani, sheria zake zivunjwe hakuna yeyote awe kiongozi wa dini atakaye amuru vita, mpaka amri ya Allah ishuke. Jambo hili haliwezekani kwa dola lolote au kwa asiye na imani ya dini madhubuti.

Historia ndivyo inavyoonyesha kuwa Manabii hawakuruhusiwa kupigana mpaka pale amri ya Allah iliposhuka. Nabii Musa[as] hakupambana na firauni kwa muda mrefu mpaka pale amri ya kupambana ilipoteremka kwake. Hapo unapata pia habari ya Nabii Daudi[as], Nabii Suleiman[as] n.k

*Endelea uk. 11*

# Matembezi ya Baiskeli Kuadhimisha Mwana Aliyeahidiwa

Na **Mwandishi Wetu**





Tanzeem ya Khuddamul Ahmadiyya Tanzania, katika kuadhimisha siku ya Mwana Aliyeahidiwa inayofanyika kila tarehe 20 ya mwezi Februari inaanda matembezi ya baiskeli yatakayofanyika jjijini Dar es salaam siku ya tarehe 17. Matembezi hayo yanakadiriwa kushirikisha Khuddamul Ahmadiyya wa Mkoa wa Dar es Salaam na mikoa ya jirani yatakuwa na lengo la kuhamasisha amani katika nchi yetu. Matembezi mahususi kuenzi neema ya Allah juu ya dini yake ya Islam kwa kuleta Mwana ambaye ameleta mageuzi makubwa ya maisha yetu ya kiroho. Tunafanya matembezi hayo kwa heshima ya nchi yetu na mchango wa Mwana Aliyeahidiwa juu ya ukombozi wa Taifa letu, kilisema chanzo muhimu cha maandalizi ya matembezi hayo ya baiskeli. Uhuru wa nchi hii uliratibiwa katika zama za Ukhalifa wa Mwana Aliyeahidiwa, harakati na watu waliohusika walikuwa na maelekezo ya moja kwa moja ya Mwana Aliyeahidiwa hivyo Khuddam tuna kila sababu ya kuhamasisha amani ya nchi yetu kupitia matembezi hayo na maadhamisho haya. Kilisema chanzo hicho. Hii Khuddamul Ahmadiyya kufanya matembezi ambayo yanaleta hamasa kubwa katika jiji la Dar es Salaam katika kuenzi amani. Allah awezeshe malengo hayo kutimia kwa maslahi ya nchi yetu. Kupenda nchi ni sehemu ya imani. Kuenzi amani ni wajibu wa kila mfuasi wa Islam.

Baada ya zoezi hilo la baiskeli na matembezi ya amani litafuatia tukio la uchangiaji wa damu utakaofanyika katika Makao Makuu ya Jumuiya ya Ahmadiyya Masjid Salaam. Zoezi hilo litaratibiwa na uongozi wa damu salama wa kanda ya Mashariki.

Siri ya Amani ya Tanzania uk. 4

# Mapenzi ya Mungu

## Maoni ya Mhariri

## MUNGU IBARIKI AFRIKA

Afrika ni bara pekee lenye matumaini mitazamo mipya duniani, ni bara ambalo bado liko na mengi mapya na mazuri kwa siku za sasa na siku zijazo. Kama anavyosisitiza **Khalifa tul Masih V (atba) Hadhrat Mirza Masroor Ahmad.** Ingawa historia ya bara hili kwa miongo mingi haikuwa ya kupendeza sana, hivyo waandishi na watu wengi wa nchi za magharibi, wakawa na mitazamo mibaya sana kuhusu Afrika.

Wengi wakiliona kuwa ni bara lenye mashaka na matatizo mengi, hasa umasikini, ujinga na maradhi, vita vya wenyewe kwa wenyewe, mashaka ya kisiasa na kiuchumi, kung'ang'ania madaraka, ugomvi na visasi. Ilimradi kila mtu aliliona bara hili kuwa ni bara la giza na lililosahaulika au lililoachwa nyuma kimaendeleo na kusahaulika kabisa.

Lakini katika siku za hivi karibuni, bara hili tukufu, limekuwa likiidhihirishia dunia kuwa ndio bara pekee na lenye matumaini makubwa ya kufanya mabadiliko katika siku za usoni, siku zijazo ambalo huenda likawa ni mfano wa kuigwa na mabara mengine duniani. Ni kweli wao wameendelea na wana mifumo yao ya demokrasia, lakini ukweli ni kuwa hata sisi katika Afrika tuna uwezo wa kuwa na demokrasia ya aina yetu na tukawa na jamii nzuri yenye maendeleo.

Kumekuwa na mabadiliko chanya katika nyanja mbalimbali, tukianza na za kiafya, kijamii, kiuchumi na hata za kisiasa. Nchi nyingi za Kiafrika zimepiga hatua kubwa za kimaendeleo katika maswala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na hata kisiasa.

Leo tutaangalia kidogo tu kisiasa katika bara la Afrika hasa kwenye swala la madaraka na kubadilishana uongozi wa juu wa nchi. Ukiachilia mbali nchi kama Tanzania ambayo utamaduni wa kubadilishana madaraka ni jambo la kawaida bila uvunjifu wowote wa amani, nchi nyengine kadhaa ambazo hazikuwa na sifa hii nazo kwa sasa zimeingia katika utamaduni huu adhimu. Liberia inakuwa mfano wa kuigwa pale ambapo baada ya machafuko mengi na umwagaji mkubwa wa damu, hatimaye Mama msomi mkubwa kabisa katika nchi hiyo **"Elen Johnson Sirleaf"** aliyeongoza nchi hiyo kwa vipindi viwili vya kikatiba aliachia madaraka baada ya kufanyika uchaguzi uliokuwa huru na haki, uliomuweka madarakani mchezaji mpira wa zamani **"George Opong Weah"** kuwa rais wa nchi hiyo. **"Elen Johnson Sirleaf"** mbali ya sifa nyingi alizojipatia mama huyo wakati wa uongozi wake, lakini pia alishinda **"TUZO YA MO IBRAHIM"** tuzo ya amani na utawala bora barani Afrika.

Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo ni miongoni mwa nchi zilizokuwa na sifa mbaya mno barani Afrika. Hasa kung'ang'ania madaraka na vita vya wenyewe kwa wenyewe. Ni dhahiri ya kwamba, nchi ya Jamhuri ya Kongo ni nchi iliyobarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini na sababu hiyo nchi hiyo ilipojipatia uhuru kutoka kwa Wabelgi, Waziri Mkuu wa kwanza mzalendo wa nchi hiyo "**Patrice Emelsy Lumumba"** alitangaza ya kwamba mali ya Kongo lazima iwanufaishe Wakongo kauli hiyo ilimjengea maadui wengi na Marekani na nchi za kibepari, zikamuunga mkono "**Moise Tshombe"** kuleta machafuko katika nchi hiyo.

Ni kweli machafuko yalikuwa makubwa na hatimaye "**Patrice Lumumba"** akauawawa. Lakini maumivu ya Kongo hayakuishia hapo, nchi ilichukuliwa na Kukungwendo Wazabanga na nchi ikanyonywa kweli kweli. Kwa hiyo mabadiliko ya hivi sasa yanamuweka Rais anayemaliza muda wake **Joseph Kabila Kabange** aliyetawala nchi hiyo kwa kipindi cha miaka takriban 18, anaondoka madarakani akiwa ameacha sifa kubwa mbili, ya kwanza ni kuandaa na kufanya uchaguzi mkuu katika nchi hiyo kubwa bila kuchukua msaada au ruzuku yeyote kutoka nchi za nje.

Ya pili pamoja na kumchagua mgombea kutoka katika chama chake, "**Emmanuel Ramadhan Shadari"** lakini amekubali kushindwa na kumuachia nchi mtoto wa hasimu wake wa siku nyingi kisiasa **"Etienne Tshisekedi wa Mulumba"** mtoto wake Mheshimiwa **"Felix Antony Tshisekedi Chilombo"** kuongoza nchi hiyo kubwa katika ukanda huu, nchi yenye utajiri mkubwa wa rasilimali za madini duniani.

Huu ni mwanzo mzuri wa Afrika mpya, Afrika ambayo tunaamini baada ya muda itakuwa mfano mwema wa amani na utulivu, hivyo kuondoa dhana ya muda mrefu kuwa hili ni bara jeusi na la giza kama ambavyo waandishi na watu wengi wa kimagharibi walizoea kuliita. Taratibu imani hii itafutika na kujenga fikra mpya kwa watu waliokuwa na mitazamo hasi kuhusu bara hili. Wao wataendelea kuliita bara la Afrika majina yote wanayatoka ila kwetu sisi Afrika ni nyumbani. Mungu Ibariki Tanzania, Mungu Ibariki Afrika.

# Wamwera Akumbusha



*Mzee Khamis Sultan Wamwera*

Kwa Jina la Allah, Mwingi Wa Rehema, Mwingi Wa Ukarimu.

Kwa Mudir Mapenzi ya Mungu

Assalaam Alaykum Warahmatullah Wabarakatuhu.

Ama baadu, kwa fadhila za Allah, Azza Wajalla, nimesoma toleo Maalum lakuadhimisha miaka 82 ya Gazeti la *Mapenzi Ya Mungu* tangu lianzishwe mnamo mwaka 1936. Neema limaula. Ninaona, bali ninaamini tumechimba na kuweka msingi mkubwa wa historia ya Jamaat Ahmadiyya nchini mwetu Tanzania. Kwa hiyo, sina budi ila kukupa wewe kongole pamwe na wale wote ulioshirikiana nao hadi kutuletea kizuri namna hii. Hii ni shughuli adhimu inastahili heshima. Bila shaka nahisi haikuwa kazi nyepesi, lakini mwishoni kwa msaada wa Allah, matokeo yakazi yenu imetuletea tunu adhimu. Allah Asisite kuwalipa ujira mwema kwa shughuli yenu hii. Awalipeni kheri na baraka tele. Awajaze elimu na fahamu. Amin thumma Amin.

Pamoja na haya, ninashauri ni vizuri kama kila mwanajumuiya apate nakala moja ya toleo hili maalum. Ni toleo miongoni mwa matoleo muhimu yanayoelimisha na kuwaelewesha watu kule tulikotoka na wenzetu hao wa mwanzoni walikumbana na mikasa gani. Huu ni utaratibu wa Qur'an Tukufu. Qur'an Tukufu inatupasha mambo mbalimbali ya manabii waliopita zamani ili sisi tunaosoma hivi sasa tuelemike kwa yale yote yatakayojitokeza. Wakati wote muumini anajifunza na kwa kweli hahitimu hadi pale kifo kimfikiampo. Hili moja li wazi sana. Allah wakati wote huwapa msaada wa ushindi waja wake juu ya maadui wao. Popote patakapokuwa pametapakaa uhasama, kisokorokwinyo na uwadui wa namna kwa namna, daima Allah huwasaidia Manabii wake pamoja na wafuasi wao. Ndivyo historia inavyonena. toka kwa Seyidna Adam[as] hadi kwa kwa bwana wetu mtukufu wa daraja Mtume Muhammad Mustafa[saw].

Ndivyo hivyo ilivyojiri, bali hali hii itaendelea kujiri kwa wafuasi wa Masihi na Mahdi Ghulam Ahmad[as] wa Qadiyan. Kila wakati wapinzani watajaribu na kujitahidi kutaka kupunguza nguvu na uwezo wa Ahmadiyya, lakini hilo halitowezekana. Daima adui ataanguka mieleka ya ajabu na kulala chali kama mende! Allah ataangaza Nuru ya Islam kupitia Ahmadiyya,



*Sheikh Kaluta Amri Abedi (aliyeketi kulia) akiwa na wanafunzi wake wa Madrasa Ahmadiyya 1957*

mwenye masikio na asikie kauli hii.

Naam, sasa ndugu Mhariri, naleta kwako yangu machache yakiwa kama nyongeza tu katika yale mazuri mliyotuletea. Tafadhali yatowe kwenye Mapenzi Ya Mungu.

Kuhusu waliowahi kutumikia *Mapenzi Ya Mungu*.

Pamoja na ukurasa wa 7 na 8 wa toleo maalum kujazwa taswira za picha za wale waliowahi kutumikia Mapenzi Ya Mungu, lakini



*Sheikh Mubarak Ahmad Ahmadi HA*

sikupata kuona picha ya Mwl. Hemedi Feruzi Mbyanana Mwl. B.K Kheri. Tuwakumbushe wasomaji wetu watukufu kwamba hawa pia walihudumia Mapenzi ya Mungu.

Jamia Ahmadiyya Tanzania: Hili ni la uhakika kabisa kwamba Chuo chetu cha Jamia Ahmadiyya katika Tanzania kina tarekhe ndefu hivi kwamba tunajivunia. Kwa mara ya kwanza Maulana Sheikh Mubarak Ahmad H.A aliidhinisha chuo hiki kufunguliwa. Kwa msaada wa Allah, mnamo mwaka 1958 chuo kilianzishwa mjini Dar Es Salaam chini ya uongozi wa Sheikh Kaluta Amri Abedi mara tu aliporejea kutoka masomoni kule Rabwah Pakistani. Mwaka huo chuo kilikuwa na wanafunzi wanne tu. Hao walikuwa Seif Mohammad Ndambwe kutoka Dar es salaam, Tatawe Mussa kutoka Kigoma, Bwana Mbwana Shamte Nyengo na Bwana Juma Abdullah Mpitakunza kutoka Rufiji. Mungu bariki, mwaka 1959, chuo kikawa na wanafunzi wa shughuli za ubashiri vijana 14. Nao ni kutoka Rufiji, Tabora, Kigoma, Moshi, Lindi na Dar es Salaam yenyewe. Mwanafunzi mmoja alikuwa ametoka Lubumbashi kule nchini Kongo sasa Jamhuri ya Kidemokrasia.

***Historia ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania***:

**DAR ES SALAAM:**

kwenye kipengele hiki, napenda tu kukumbusha hili. Pamoja na kutaja majina matatu ya watu wa kwanza kujiunga katika Ahmadiyya mjini Dar es Salaam, bali pia walikuwepo Bwana Athmani Mtipuka, Mwalimu Kombo Nyange, Bwana Seif Mohammed Ndambwe, Dhahiri Mdiwila na Bwana Saidi Ally Kimemeneki na Bwana Mlemwa N. Legeza.

**MOROGORO**:

Pamwe kuwataja Mzee Rashidi Msabaha na Mzee

*Endelea uk. 3*

BODI YA UHARIRI

**Msimamizi:** Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
**Mhariri:** Mahmood Hamsin Mubiru.
**Kompyuta:** Ahmad Abdul Nasibu.
**Mchapishaji:** Sheikh Bashart Ur Rehman
**Msambazaji:** Mwl. Omari Ali Mnungu
**Wajumbe:**
1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Dr. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
**Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.**
**Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.**
**Email: mapenziyamungu36@gmail.com**

# Wamwera Akumbusha

*Kutoka uk. 2*

Chamchua Milonge, lakini pia palikuwepo ndugu wengine pia ambao walijiunga katika Ahmadiyya mapema mno. Nao ni Mzee Ally Ramadhani na Ramadhani Abdullah ambao walikuwa ni wenyeji wa kule Lugala Mazimbu.

**LINDI**: JAMAAT YA TATU MASHUHURI IMESAHAULIWA

Lindi ni mkoa ambao humo Jumuiya ya Ahmadiyya iliingia zamani sana. Kwa bahati mbaya toleo maalum la kuadhimisha miaka 82 ya Mapenzi ya Mungu, historia imesahau!. Kwa hiyo, naona kuna umuhimu wa kukumbushana. Ni katika mwaka wa 1950, Sheikh Fadhillah Bashir alipofika Lindi kuwakilisha taarifa za ufikaji wa Seydna Ahmad[as], akiwa Masih na Mahdi wa Mtukufu Mtume wetu Muhammad[saw]. Wakazi wa Lindi walielezwa kuwa utume ni neema kama zilivyo neema zingine kutoka kwa Allah. Wanadamu huomba neema mbalimbali kutoka kwa Allah. Kama vile chakula na maisha bora, basi utume ni miongoni mwa neema kubwa ya kumuongoza mwanadamu kumtambuwa Allah wake. Pamoja na hilo, ndugu wa Lindi pia walielezwa kifo cha Nabii Issa[as] na uchafu wa mahirizi, kupiga ramli, matanga na karamu.

Allahu Akbar, maelezo haya yakawasha moto katika mioyo ya Masheikh wa Sunni. Kwa hiyo wakawatahadharisha wafuasi wao kamwe wasiambatane na Sheikh wa Ahmadiyya kwa sababu atawapoteza kwa kuwatoa katika Islam. Lakini panapo ukweli siku zote uwongo hujitenga. Upepo wa ukweli masikioni mwa baadhi ya wateule wa Allah yakasikiliza kwa makini maneno yaliyokuwa yanatokana na Sheikh wa Ahmadiyya. Hao hawakuwa na namna nyingine ila kujiunga katika Ahmadiyya. Waliojiunga wakati huo alikuwa ni Sheikh Mahadhi Mwinyishaweji na



*Mzee Dungurusi*

Sheikh Khalid Mataja wa Mingoyo. Sheikh Ahmad Mataka Busra na Mzee Ismail Ahmad Mpukutile kutoka Lindi mjini. Wengine walikuwa Sheikh Issa Haruna Kurunguja na Mzee Abdullah Mshamu Dungurusi.

Masheikh Wasuni walipoona yao hayakusadifu na kutiwa maanani, wakabuni mambo mbalimbali ya usumbufu kuwatesa wanajumuiya. Hata hivyo, Sheikh Fadhillah Bashir aliwaambia masheikh Wasuni kwambakamahawataachakuwakatili Waahmadiyya, watamweleza Subhana Wataala jambo hilo na yeye Anajuwa Atakachofanya. Masheikh Wasuni walibeza na kucheka sana juu ya hili hata ikabidi baadhi ya wanajumuiya wahame kutoka Lindi hadi Rufiji ambako huko walipokelewa vyema mno na ndugu zao wa imani. Muhajirina hao ni Sheikh Issa Haruna Kurunguja, na Mzee Abdullah Mshamu Dungurusi na familia zao.

Lahaula! Huko nyuma Allah mkubwa na mwenye uwezo, Afanyaye Apendavyo, Akapeleka Lindi kimbunga chenye upepo mkali ambacho kiliweza kuangusha miti, kikang'oa minazi na kubomoa baadhi ya nyumba, bali kiliteketeza watu pia.

**RUFIJI:**

Ndugu Mhariri, nimeshangazwa sana kuona hata Jamaat ya Rufiji haikupata bahati ya kuingizwa kwenye historia. Maskini we imesahauliwa! Si kitu, kwa kuwa tupo baadhi ya watu tulikuwepo wakati Jamaat hiyo inaanzishwa, basi tutaelezana japo kwa uchache mambo yalikuwaje.

Ninakumbuka vizuri sana, ni katika mwaka 1955 wakati wa Sheikh Swaleh Mbaruku Kapilima akitokea Dar es Salaam kuelekea kwao Njinjo Wilaya ya Kilwa. Alipanda gari lililomfikisha kijiji cha Nyipara, Tarafa ya Rusende Wilaya ya Rufiji. Nyipara ni kijiji ambacho kilikuwa na watu wanaopenda sana dini. Wakati wa ujahiliya ng'ombe mmoja alikuwa anaanguka mfungo sita kwa ajili ya ziara. Na Sheikh Swaleh alifika hapo katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani na hakujaaliwa kupata gari kwa haraka kuelekea Kilwa. Basi akabaki Nyipara karibu siku kadhaa hivi akisubiri usafiri. Katika wiki hizo chache, sheikh Swaleh alipata nafasi nzuri ya Tabligh. Aliwaeleza wana Nyipara jinsi hali ya Waislamu ilivyo hivi sasa. Aliwaambia kuwa Waislam wamefikia hatua ya kuamini imani ya kikristo bila ya wao wenyewe kujielewa!. Kwa mfano, Sheikh aliwaambia: Imani ya kuamini Issa[as] yuko mbinguni si ya Islam. Uislam unafundisha kwamba tumezaliwa hapa duniani, tutaishi hapa na tutafia hapa hapa.

Hapo kabla wana kijiji cha Nyipara na Waislamu wa sehemu nyingine waliambiwa na masheikh wao kwamba kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani haujuzu kabisa mtu usiku wala mchana kumgusa mkewe. Tendo la ndoa litafanyika mara tatu tu kwa mwezi mzima wa Ramadhani. Kumi la kwanza siku moja, kumi la pili siku moja na kumi la mwisho siku moja. Lakini Sheikh Swaleh akawaambia kuwa hivyo sivyo. Akawafungulia Qur'an Tukufu na kuwaonesha kauli ya Allah Anavyosema. Ananena: "*Mmehalalishiwa usiku wa swaumu kuingiliana na wake zenu, wao ni nguo kwenu na ninyi ni nguo kwao. Allah amekwisha jua ya kwamba mlikuwa mkijihini nafsi zenu, kwa hiyo Amewaelekeeni na kuwasameheni, basi sasa laleni nao na takeni Aliyowaandikieni Allah. Na kuleni na kunyweni mpaka ubainike kwenu uzi mweupe katika uzi mweusi wa alfajiri, kisha timizeni swaumu mpaka usiku.Wala msilale nao na hali mnakaa misikitini. Hiyo ndiyo mipaka ya Allah, basi msiikaribie. Hivi ndivyo Allah Anavyobainisha Aya zake kwa watu ili wapate kumcha*" (Sura Al Baqara:188).

Sheikh Swaleh Mbaruku pia hakusita kuwaeleza wenyeji wa Nyipara umuhimu wa kuendelea utume na utaratibu wa Ukhalifa katika Islam. Zama zetu hizi Seydna Ahmad wa Qadiyan amefika akiwa Masihi na Mahadi. Akawahimiza kila mtu kujiunga naye . kwa tangazo hilo, robo tatu ya wakazi wa Nyipara, wanaume kwa wanawake wakafanya baiat na kujiunga katika Ahmadiyya. Ndugu Mhariri, niwie radhi niwataje wachache sana kwa niaba ya wengine. Katika mwaka 1955, watu waliojiunga katika Jamaat Ahmadiyya ni pamoja na Bwana Maliki A. Mbungiro (Watachoka) ambaye alikuwa mshairi mahiri. Bwana Juma A. Mpitakunza ambaye naye pia alikuwa mshairi mzuri sana. Bwana Rashid S Njoka aliyekuwa Karii mzuri wa Qur'an Tukufu. Bali huyi alikuwa na swifa nyingine. Alikuwa twayari wakati wowote kupigana na yeyote atakaefanya nyokonyoko kwa kukashifu Ahmadiyya. Alikuwa mstari wa mbele kuwalinda wanajumuiya.



*Mhenga Rajabu I. Mkoga*

Wengine waliojiunga katika Ahmadiyya mwanzoni ni Mzee Mchawi Ndugu Matimbwa, Mtindasi Kisoma, Mzee Husein Shamte Nyengo, Mzee Mhenga Rajabu Ibrahimu Mkoga, Mzee Msongoro Magenge, Mzee Salum Mbungiro na Mzee Yusuf Mbungiro. Mzee Omari Salum Mbonde (Mzungu) ambaye aliwahi kwenda vitani mnamo mwaka 1939-1945 ambaye inahesabiwa kuwa vita ya pili ya dunia. Alikuwa mtanashati na swifa ya umaridadi. Kulikowako Mzee Mussa Sungu Matimbwa na Bwana Seif Sungu, Salum Adam na Mzee Omari Lihenga. Mzee Ramadhani Ngirini na Bwana Mwinyihija Ngirini. Mzee Sultan Shamte Wamwera na mdogo wake Bwana Swaleh Shamte Wamwera. Mzee Abdullah Sozigwa na wanaye wawili: Bwana Uwesu Sozigwa na Bwana Jafari Sozigwa.



*Shabani A. Malinda*

Kama nilivyotamka hapo kabla kwamba orodha ni ndefu si rahisi kuandika hapa yote. Waila sasa nataka nimalizie kutaja majina ya wazee wengine hapa chini. Ndugu wengine waliojiunga katika Ahmadiyya mnamo mwaka 1955 ni Mzee Shaabani Athumani Malinda, Mzee Ally Abdulrahman Nyamkwasu, Bwana Kassimu Rajabu Mkoga, Mwalimu Ibrahimu Rajabu Mkoga, Saidi Omar Mkoga na Bwana Saidi Ngakonda.



*Ibrahim R Mkoga*

Naona ni vyema pia nikawataja akina mama wa mwanzo katika kujiunga na Ahmadiyya kule Rufiji mnamo mwaka huo wa 1955. Akina mama hao mashujaa pia walikuwa wengi kiasi hiki kwamba kutakuwa vigumu kuwaratibu hapa wote. Bali nitawataja hapa wachache kwa niaba ya wale wengine. Historia ya Jamaat ya Rufiji haiwezekani kumsahau Bi Mariyamu Mohammad Mpapu ambaye alionesha ujasiri mkubwa sana wakati wazazi wake walipomfikia na kumtaka aache Ahmadiyya na arudi katika usuni, kwa sababu ati Jumuiya hii si ya Kiislamu. Lakini yeye kwa heshima na taadhima aliwaambia wazazi wake kwamba hakufanya kosa la jinai kujiunga katika Ahmadiyya na Jumuiya haipo nje ya Uislamu. Wazazi wa bi Mariyamu walisema kwamba wao wameambiwa na Masheikh wao kuwa Waahmadiyya ni makafiri wala si Waislamu. Msahafu wao una juzuu 31 kisha wana Mtume wao. Kwa hiyo siku ile walifika kumchukua asibaki kwenye ukafiri. Walimlazimisha atoke kwa mumewe waende naye kwao wamnusuru katika kuritadi dini. Mariyamu aliamriwa kwa nguvu atoke kwa mumewe na kama hakufanya wanavyotaka wao, basi watamkosea radhi.

Bi Mariyamu Muhammad Mpapu kwa kuwa alikuwa na hakika na kile kitu alichokikiri, akasimama imara. Akawaambia wazazi wake kuwa yeye hataondoka kwa mumewe kwa sababu zile zilizotolewa na wazaziye, kwa sababu zilikuwa hazina mashiko. Akawaambia wazazi wake kwamba Ahmadiyya si dini mpya wala haina Qur'an Tukufu yenye juzuu 31. Wapinzani wa Hadhrat Muhammad[saw] waliambiwa walete sura moja tu inayofanana na hii, na waite watu wengine wasaidiane kutenda jambo hilo. Wapinzani waliambiwa kamwe hawatoweza basi watambuwe hawataweza kamwe; waogope moto ambao kuni zake ni watu na mawe nao huo umeandaliwa kwa makafiri. Bi Mariyamu akawauliza wazaziye kwa heshima; Ikiwa wale wa zamani walishindwa kuleta sura moja tu inayolingana na Qur'an Tukufu, Jumuiya ina uwezo gani zaidi wa kuleta juzu moja kamili? Masheikh wenu Wasuni wanasema uwongo. Wazazi wa Bi Mariyamu wakanuna. Walikasirika sana, wakamkosea radhi na kutamka tangu siku ile si binti yao tena. Kwa msaada wa Allah Bi Mariyamu Muhammad Mpapu amefariki mwanzoni mwa mwaka 2018 baaada ya kuishi duniani miaka 85.

Anayefanana na Bi Mariyamu ni Bi Tatu Hassani Maunga. Huyu alijiunga katika Ahmadiyya mnamo mwaka 1956. Wazazi wake waliposikia binti yao amejiunga katika Ahmadiyya, haraka sana wakafika kwake kwa nia ya kumchukua na kumrejesha kwao. Walichukua hatua hiyo kwa sababu Masheikh wao waliwaambia kuwa Waahmadiyya ni makafiri si Waislamu. Binti aliwakaribu vizuri wazaziye. Wazee wake wakatamka kwa kumwambia kwamba wao wamefika pale kwa nia ya kumchukua ili arejee kwao, kwani kama ataendelea kubaki kwa mumewe ataendelea kupotea na kuuacha Uislamu. Bi Tatu Hassani Maungo aliwahakikishia wazazi wake kwamba Ahmadiyya si dini mpya, bali ni silsila iliyo sawa kabisa ambayo kila mtu anatakiwa kujiunga nayo. Aliwaambia wazi

***Inaendelea uk. 4***

# Wamwera Akumbusha

*Kutoka uk. 3*

kuwa kutojiunga ni hasara tena hasara kubwa. Wale wakamuuliza ni hasara gani? Bi Tatu akawapa jibu kwa kuwaambia hasara yenyewe ni kutoelewa mafundisho sahihi ya Islamu. Kwa mfano, aliwaeleza wazaziye, ninyi wazee wangu mlichukua shilingi 300/= za mahari yangu, wakati hizo zilikuwa ni haki yangu. Ingekuwa sawa kama mimi mwenyewe ningewapeni kwa ridhaa yangu. Lakini ninyi mlitwaa kwa sababu ya wazazi.

Bi Tatu Hassani Maunga aliwaambia wazazi wake ufikaji wa Seydna Ahmad[as] akiwa Masih na Mahdi katika zama hizi. Aliwathibitishia kuwa kulala matanga, hitima, karamu na mahirizi ni miongoni mwa amali ya shaitwani ambayo ni mambo waumini wanatakiwa kuyapa kisogo. Baada ya maelezo haya, huyu binti alitayarisha chakula kwa ajili ya wazee wake hao, lakini walikasirika na kwa hasira walisusa hata kula.

Huyu hapa mwingine ni Bi Hawa Saidi Machela ambaye alikuwa ni mke wa Mzee Ally Abdulrahman Nyamkwasu. Naye alifikiwa na wazazi wake kuja kumchukua baada ya kupata tu habari kuwa binti yao ameshajiunga katika Ahmadiyya. Pamoja walikuwa na ghadhabu iliyochanganyika na hasira, lakini binti yao, kwa hekima aliweza kuteremsha kiwango cha mfundo huo. Walitulizwa kwa maelezo mazuri sana ya busara na hekima kutoka kwa binti yao. Wazee hao waliambiwa dini ni Islam na Ahmadiyya ni Jumuiya iliyoanzishwa na Seydna Ahmad[as] kwa amri ya Subhana Wataala. Wazee hao walirejea kwao bila ya kutekeleza lililowapeleka pale.

Ukiachilia mbali akina mama hawa watatu, pia walikuwepo akina mama wengine wengi waliojiunga mwanzoni mwa mwaka 1955. Kwa kuwanukuu majina yao hapa, nitataja machache. Alikuwepo Bi Sofia Abdullah Mbungiro na Bi Kesi Salum Mbungiro. Bi Zabibu Mussa Sungu, Bi Sofia Mussa Sungu na Bi Habiba Mussa Sungu. Bi Zainabu Shamte Nyengo na Bi Khadija Nyamailo. Bi Zainabu Saidi Ngunde na Bi Maimuna Yusuf Ndete. Bi Salima M. Ngirini, Bi Zainabu M. Ngirini pamoja na Bi Moza Ramadhani Ngirini.



*Bi Khadija Nyamailo*

**MACHAME-MOSHI:**

Naam, ni kweli kabisa kwamba Machame kuna historia nzuri ya kusisimua mioyo yenye imani ya dini. Ni katika mwaka wa 1956, pale Moshi mjini palikuwa na duka likiitwa Mombasa Bookshop. Ni duka la vitabu na magazeti ambalo lilimilikiwa na mfanyabiashara mmoja wa kihindi. Siku moja, mwalimu Elibariki Shaabani Shoo akitokea Machame aliingia dukani hapo na kuona maandiko mbalimbali. Punde macho yake mawili yakaona Gazeti la Islamu lililoandikwa kwa herufi kubwa MAPENZI YA MUNGU. Nafsi yake ilimshawishi alinunue na alisome ili ajue ndanimwe mu nini. Kwa wakati ule hilo lilikuwa Gazeti pekee la Islamu kuchapishwa. Akalinunua na kwenda nalo nyumbani kusoma.



*Mwl Elibariki Shaban Shoo*

Mwalimu Shaabani kufika nyumbani tu, kwa hamu na shauku akaanza kulisoma gazeti hilo. Aliyokutana nayo humo ndani, alilazimika kumwandikia Maulana Sheikh Mubarak Ahmad H.A kule Nairobi Kenya wakati huo yeye ndiye Mhariri Mkuu wa *Mapenzi Ya Mungu*. Kwa muda wakawa wanaandikiana, baadaye, Maulana Sheikh Mubarak Ahmad na Sheikh K.Amri Abedi kwa pamoja walifika Machame Moshi kwa nia ya tabligh. Ni siku ngumu naweza kusema hivyo. Mwalimu Shaabani akishirikianana nduguze walitayarisha kongamano la nguvu kuzungumzia mambo mbalimbali ya dini yetu ya Islam. Masheikh Wasuni walitaarifiwa kuwa patakuwa na mazungumzo ya aina hiyo. Palitayarishwa pahala pa kukutana na kwa kweli watu wengi walihudhuria.

Masheikh wetu walizungumza juu ya haja ya kuendelea kwa Utume, ufikaji wa Seydna Ahmad[as] akiwa Masihi na Mahadi, kifo cha Nabii Issa[as] na umuhimu wa kujiunga katika Jamaat Ahmadiyya. Masheikh Wasuni walikuwepo kwenye hadhara hiyo, lakini hakuna aliyethubutu kujitokeza kupinga chochote katika yale yaliyoelezwa. Masheikh wa Jamaat Ahmadiyya walikaa Machame siku mbili wakibashiri watu mbalimbali.

Maulana Sheikh Mubarak Ahmad na Sheikh K. Amri Abedi walipoondoka Machame na kurudi Nairobi Kenya, nyuma huku waalimu na masheikh Wasuni wakaanza kuwashawishi watu eti wasiwasikilize Ahmadiyya kwani hao ni makafiri si Waislamu, wana mtume wao. Maneno hayo yaliyojibiwa na baadhi ya wafuasi wao kwamba kwa nini sasa mbona hawakusema wakati Masheikh wa Ahmadiyya walipokuwepo hapo! Masheikh wao walikuwepo petu hapa takribani siku mbili, ninyi Masheikh wetu hamkusema kitu, leo wameondoka mnasema tusiwasikilize! Kwani wapo wapi sasa!

Wakazi wa Machame wakatafakari sana. Baada ya kutafakari wakaona ukweli uko wapi. Ndugu wengi wakajiunga na Ahmadiyya, ukoo wa akina Shoo ukiongoza. Mwaka 1956 waliojiunga alikuwa Mwalimu Elibariki Shaabani Shoo, Mzee Ibrahimu Seif Shoo, Mzee Abdu Seif Shoo, Mzee Ally Seif Shoo, Mzee Idrissa Issa Shuma, Mzee Adamu Maiyo, Mzee Adnani Massawe na Mzee Imran Kweka.

Ni kweli historia hujirudia. Tunasoma kwamba zama za Bwana wetu Mtukufu Mtume Muhammad[saw] wakati amri ya kuwakataza kunywa pombe iliposhuka, waaminio mara moja walitii amri hiyo. Si kwamba hawakunywa tu, bali hata vile vifaa walivyokuwa wanahifadhia pombe hiyo walivunja na inasemekana baadhi ya barabara za Makka michirizi ya pombe ilionekana. Ndivyo ilivyotokea pale Machame Moshi. Mzee Imran Abdullah Mganda alipoamua tu kujiunga na Ahmadiyya akaacha kabisa kunywa pombe, kuuza na akatupilia mbali vifaa vyote walivyokuwa anavitumia katika kuhifadhia pombe hiyo. Mzee Imran huyu ndiye baba mzazi wa Mwalimu wetu Abdul Imran. Kwa hakika Allah wetu ni mwingi wa Rehema na Ukarimu.



*Wanajamaat wakongwe wa Machame: Pili kulia-Daudi Shoo, kushoto mwisho Mzee Imran A. Mganda, Nne kulia-Ibrahim Shoo, Mbele-Ahmad Okash*

Kila wakati watu kadhaa waliendelea kujiunga katika Jamaat. Baadaye kidogo, mnamo mwaka 1960, akaja kujiunga Mzee mmoja wa Kisomali - Ahmad Okash. Huyu alikuwa anaketi mjini Arusha. Mzee huyu alikuwa shababi wa imani. Alikuwa makini, mweledi na alisimama imara. Wakati wote kwenye shughuli za jumuiya alikuwa mstari wa mbele. Hakutehemu wala hakuchoka. Alijitolea muda wake mwingi kwa shughuli za Jamaat. Alijitolea kwa mengi mno wala hakuogopa kufilisika. Alinunua pikipiki na akamkabidhi Mwalimu Shaabani Shoo kwa ajili ya kazi za Jumuiya. Akajenga nyumba kule Arusha kwa ajili ya Jamaat. Hadi sasa nyumba hiyo ipo.

Mzee Okash alipokuwa hospitali anaumwa kule Nairobi Kenya, Wasomali wenziye walifika kumjulia hali. Wao walimwambia kwamba kama atafariki, hawatashughulikia mazishi yake kwa sababu ameacha ule Uislamu wa asili na akajiunga na Ahmadiyya. Mzee Ahmad Okash aliwajibu nduguze hapo kwamba atakapofumba macho na kuondoka katika dunia hii, wala wasipate taabu sana. Mwili wake wautowe nje na kuutupa porini ili kunguru, mwewe, sisimizi na mbesi wajipatie maakuli.

Ndugu Mhariri, Samahani sana kama kutakuwapo usumbufu wowote ule kwa hili.

Wasalaam, Wako,

**Khamis Sultan Wamwera**, 09/11/2018

---

Ustadh Khamis Wamwera kaonyesha njia. Kila aliye na taarifa, picha, Habari za Ahmadiyya; atuletee ili tuweze kuhifadhi Historia yetu.

Shumbe Ustaadh Wamwera!

***Mhariri***

## Je Wajua?

Je waijua siri ya amani ya nchi yetu Tanzania tunayojivunia? Isome hapa chini.

Mwalim Hemedi Mahmood Feruzi Mbyana aliona njozi mnamo siku za uhuru, labda mnamo mwaka wa sitini kabla ya uhuru au mnamo siku zenyewe za uhuru, kwamba alimuona Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad[as] akiwa jukwaani pale Mnazi Mmoja pamwe na waheshimiwa wengine wakiwa katika sherehe za uhuru wa Tanganyika. Hadhrat Ahmad[as] alikuwa ameinuka kwa juu zaidi kuliko waheshimiwa wengine waliokuwepo jukwaani kwenye sherehe hiyo. Uso wa Hadhrat Ahmad[as] ulikuwa unang'aa zaidi kuliko wengine wote waliokuwepo hapo. Mwalimu Hemedi Feruzi Mbyana macho yake alikuwa tu ameyalenga kwa Hadhrat Ahmad[as] na kutoshughulika na sherehe zilizokuwa zikirindima hapo. Alikuwa amevutiwa mno na haiba ya Masihi Aliyeahidiwa[as]. Aliendelea kumtizama hivyo hadi akaamka. Alipomuhadithia ndoto hiyo Sheikh Mubarak Ahmad, akamuambia kuwa ***kumuona Nabii wa Allah Akiwa amejumuika kwenye sherehe ya uhuru wa nchi fulani, taawili yake ni kwamba nchi hiyo itakuwa na amani itakayodumu muda mrefu.***



*Mwl Hemedi Feruzi Mbyana*

Leo Tanzania yajulikana kuwa ni Kisiwa cha Amani.

Wakati wa sherehe za uhuru, mfuasi wa Hadhrat Ahmad[as], Sheikh Amri Abedi Kaluta,



alikuwa ndiye Mkuu wa Jiji la Dar-es-salaam, akiwa Meya wa kwanza mwafrika wa jiji hilo tangu mwaka wa 1960, kabla hata ya uhuru. Yeye ndiye alimkabidhi mume wa Malkia wa Uingereza, Duke of Edinburgh, aliyekuja kuikabidhi Tanganyika kwa Watanganyika, ufunguo wa jiji la Dar es salaam.

Hadhrat Khalifatul Masih wa pili[ra] aliwahi kutamka mara kadhaa kwa watu tofauti akisema: *"**Tanganyika Hamara He! = Tanganyika ni nchi yetu!**"*.

# Tafuteni Radhi ya Allah

*Kutoka uk. 1*

sala pale ambapo ninyi mtakuwa watekelezaji wake wa kweli, kwa uangalifu mkubwa sala zenu za kila siku. Anaendelea kusema; "… kukiri na kuamini pekee hakumsaidii mtu… Allah haridhiki kwa maneno matupu. Ndani ya Qura'n tukufu Allah ameweka vitendo vizuri kuwa pamoja na Imani." Amesema "vitendo vizuri ni vile ambavyo havina aina yo yote ya ufisadi hata ule ulio mdogo.

Basi hiki ndicho kipimo, na kigezo, ambacho kama tutafuata katika mwaka wetu huu, na kama tutafanya jitihada ya kutumia uwezo wetu wote wa kupata mambo haya basi mwaka wetu huu mpya utakuwa ni wenye baraka na mafanikio. Na kama hatukufanya hivi basi kama nilivyokwishaeleza ya kutakiana kwetu heri ya mwaka mpya itakuwa ni jambo la kawaida tu. Kusali tahajjud na sala ya al-Fajiri katika usiku wa siku ya kwanza ya mwaka mpya hakiwi ni kitendo kinachoenea na kujaa mwaka mzima bali kitendo hiki kikidumu katika kipindi chote cha mwaka sawa na uwezo ndiyo wema haswa. Allah Atujaalie uwezo wa kutekeleza mambo haya yote, na kwa hakika na ajaalie mwaka huu kuleta baraka niyingi kwa ajili yetu. Nasi tuweze kushuhudia kupatikana kwa maendeleo makubwa katika Jama'at.

Baada ya haya mimi ninarudi kuzungumza hotuba juu ya madhumuni mengine. Kama vile tunavyofahamu kuwa mwezi wa Januari huwa ni mwezi wa kuanza kwa mwaka wa mchango wa Waqf-e-Jadid. Na kwa kawaida katika hotuba ya kwanza au ya pili ya mwezi wa Januari hutolewa tangazo la kuanza kwa mwaka mpya kwa mchango huu. Kwa fadhili za Allah kujitolea katika mali ni jambo la pekee katika Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na kwa nini isiwe hivyo kwani Masihi Aliyeahidiwa[as] katika zama hizi sawa na mafundisho na maelekezo ya Qur'ani Tukufu na Mtume wake s.a.w ametujaalia uelewa mpana wa hakika ya kujitolea katika njia ya Allah.

Allah Amekumbusha sehemu mbalimbali katika Qurani Tukufu juu ya kujitolea katika njia ya Allah. Jambo hili si kwa sababu Allah ni muhitaji wa mali zetu bali sisi kwa kujitolea tunapata faida sisi wenyewe na kwa ujumla wake sisi tunashuhudia maendeleo ya Jamaat, nayo inapata faida pia. Allah anasema katika Qurani Tukufu;

*Kwa hiyo Mcheni Allah mwezavyo, na sikilizeni na tiini na toeni, itakuwa heri kwa nafsi zenu; na aepushwaye na ubahili wa nafsi yake, basi hao ndio wenye kufaulu*. (64:17)

*Mkimkatia Allah sehemu nzuri, Atawazidishieni na Atawaghofirieni, na Allah ni mwenye shukurani, Mpole.* (64:18)

Kwa hiyo Allah huwa anatoa zaidi na zaidi kwa mtu yule anayezidi katika kutoa katika njia Yake. Katika utoaji huu wa michango hupatikana faida ya mtu mwenyewe binafsi na maendeleo ya Jamaat, ambayo ni njia moja wapo ya maendeleo ya mtu binafsi. Vilevile Mtume s.a.w. amesema "***Jiepusheni na kufanya ubahili, ni ubahili uliyoyaangamiza mataifa ya zamani***"

Hali kadhalika amesema katika sehemu nyingine; "Jiokoeni na moto hata kama mna uwezo wa kutoa nusu ya kokwa ya tende.

Kujitolea huku kudogo katika njia ya Allah na kwa ajili ya kupata radhi yake kunaokoa na moto. Basi kujitolea katika njia ya Allah ni kwa ajili ya faida yetu. Akikumbusha juu ya umuhimu wa kujitolea huku katika njia ya Allah Masihi Aliyeahidiwa[as] anasema; "*Haiwezekani kwenu muwe na mapenzi makubwa juu ya mali na wakati huo huo juu ya Allah. Ninyi mnaweza kupenda kitu kimoja tu*." Akasema tena; "*Ni mwenye bahati kubwa mtu yule anaye mpenda Allah, kama kati yenu kuna mtu anayejitolea mali yake kwa kumpenda Allah basi bila shaka mimi ninaamini kuwa katika mali yake kutakuwa na baraka nyingi zaidi kuliko za wengine, kwa sababu mali haziji zenyewe bali zinakuja kwa matakwa ya Allah. Basi mtu yule anayetenga sehemu ya mali yake kwa ajili ya Allah lazima ataipata. Lakini badala yake mtu yule asiyefanya huduma sawa na inavyotakiwa kufanya katika njia ya Allah kwa kupenda mali, yeye lazima mali hii ataikosa*." Yaani yatapotea. Pia anasema; "*Msifikirie kuwa mali inakuja kwa sababu ya juhudi zenu, bali inakuja kutoka kwa Allah, na msifikirie kuwa kutoa sehemu yoyote ya mali yenu au kufanya huduma nyingine ya aina yoyote mnafanya ihsani kwa Allah na Mtume Wake, bali hii ni ihsani Yake kuwa Yeye Anawaiteni Kwake kwa ajili ya huduma hii*." Anasema; "*Fahamuni kwa yakini ya kwamba kazi hii inatoka mbinguni, na huduma yenu ni kwa ajili ya heri yenu*."

Kwa fadhili za Allah moyo huu wa kufanya huduma na kujitolea katika njia ya Allah wameujua pekee watu wale wanaojiunga na Jumuiya ya Masihi Aliyeahidiwa[as] nao wameujua vizuri sana, nao wanaendelea kujitolea zaidi na zaidi. Sio wale tu waliojiunga na Jumuiya toka zamani bali hata wale Waahmadiyya wapya pia wameujua moyo huu wa kujitolea na hakika yake baada ya kufanya baiat. Wapo wale ambao huishi katika ufukara mkubwa, lakini hawataki kubaki nyuma ya wengine katika kujitolea mali, kwa hiyo wanaendelea kujitolea kama vile walivyojitolea maswahaba wa Masihi Aliyeahidiwa[as] wakati wake. Wapo walio mifano ambayo kuhusiana nao Masihi Aliyeahidiwa[as] alikwishasema wakati ule kuwa mimi ninashangaa juu ya mapenzi na ikhlas ya Jumuiya yangu, miongoni mwao kuna wale ambao hawana maisha mazuri. Kisha yeye akatoa mfano, na kusema; "*kama alivyo Mian Jamal Din, Khair Din, na Imam Din Kashmiri*" anasema; "*hawa ni watu wanaoishi karibu na kijiji changu, ndugu wote hawa wanne ambao huenda wana ujira wa jumla wa ANNA (senti) tatu au nne, hutoa na hushiriki michango yao ya mwezi kwa moyo mmoja*."

Michango ya watakatifu hawa waliojitolea wakati huo kwa ajili ya kueneza Dini leo imekuwa sababu ya watoto wao kupata maisha mazuri. Kama nilivokwishaeleza nyuma, roho ya aina hii inaonekana katika baadhi ya sehemu bali sehemu zote hadi leo, na tunaiona miongoni mwa watu wale wanaoishi mbali, ambapo wamezaliwa au wamejiunga na jumuiya miaka mia moja baada ya Masihi Aliyeahidiwa[as] na ambao hawajawahi kuonana na Khalifa lakini mapenzi ya dini, utii kwa ukhalifa na uaminifu kwa baiati na Masihi Aliyeahidiwa[as] jazba ya kujitolea kwa ajili ya dini imeongezeka kiasi cha kushangaza. Kama liangaliwe jambo hili tu linatosha kuwa ushahidi wa ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa[as] na hakuna yeyote anayeweza kuleta jazba hii moyoni isipokuwa Allah. Sasa nitatoa mifano michache ya watu waliojitolea katika njia ya Allah na jinsi Alivyo wajibu.

Bwana Rafiki Frimpong kutoka Ghana anasema; "miaka michace iliyopita nilitaka kutoa kiasi cha fedha cha pound 5,000, kipindi kile nilikuwa pia ninafanya kazi lakini mshahara wangu haukuwa mkubwa, kama ningekusanya mshahara wangu wa mwaka mzima isingeweza kufikia kisai hiki. Hata hivyo nilifanikiwa kupata mkopo wa Pound 3000 kutoka banki, na nilikuwa ninalipia deni asilimia 40 ya mshahara wangu katika kila mwezi, lakini hata hivyo nilikuwa pia ninalipia mchango wangu wa kila mwezi kikamilifu sawa na mshahara wangu. Wala sikujali asilimia ile 40 iliyotoka. Anasema siku moja nilienda katika mission ya Kumasi (Kumasi ni mji mmoja wa Ghana), mbashiri wa eneo lile akanikumbusha juu ya mchango wangu wa Waqf e Jadid. Wakati ule ule nikaingiza mkono wangu kwenye mfuko na kukuta kiasi cha fedha cha mchango wangu, lakini nikafikiria kuwa nikitoa kiasi hiki cha fedha kwa ajili ya mchango, sitabakiwa na fedha kwa ajili ya kwenda kazini katika siku zilizobaki. Anasema hata hivyo mimi nikatoa kiasi hicho kwa ajili ya mchango. Nilikuwa ninarudi nyumbani nilipopata ujumbe katika simu yangu ya kuwa kuna kiasi fulani cha fedha kilichoingia katika akaunti yangu ambacho kilikuwa mara tano zaidi ya kiasi kile nilichotoa mchango. Kama vile alivyokwishasema Masihi Aliyeahidiwa[as] kuwa Allah anarudisha kwa kuzidisha zaidi na zaidi. Mimi nikadhani huenda watu wa benki wamefanya makosa kuweka kiasi hiki kwenye akanti yangu nao watakirudisha baadaye, kwa sababu mshahara wangu tayari ulikwishaingia. Lakini siku iliyofuata nilipokwenda kazini nikafahamu kuwa kiasi hiki kilikuwa ni baki ya miezi ya nyuma. Kwa hiyo mimi nikamshukuru Allah, Allah pamoja na hofu niliyokuwa nayo amenijaalia uwezo wa kutoa mchango wangu. Kuanzia siku ile nimekuwa makini katika kutimiza ahadi na kutoa michango yangu ya kila mwezi. Bwana huyu ni kutoka katika bara la Afrika anayeishi nchi ya mbali.

Burkina Faso ni nchi nyingine mojawapo ya Afrika, ambayo ni miongoni mwa nchi zinazozungumza Kifaransa. Mbashiri wa kule Bobo Dioulasso anaandika, hili ni jina la mji wa kule, kwamba kijana mmoja mwanajumuiya mpya aitwaye Bw. Zodi ameishi na wasiwasi mkubwa kwa muda fulani kwa sababu ya ugonjwa wa akili, na alikuwa anatumia vidonge vya usingizi, akachanganyikiwa. Na hali hii ikazidi zaidi. Siku moja akaja kwenye nyumba ya mbashiri, na akauliza mchango wake wa Tahrik Jadid na Waqf Jadid ni kiasi gani? Anataka kutoa. Mbashiri wa pale akamwambia wewe toa kiasi chochote sawa na uwezo wako. Yeye akauliza tena mchango halisi ni kiasi gani? Mbashiri akamwambia naye kwa furaha akatekeleza na kuondoka. Baada ya siku chache akaja tena, na kusema kuwa mimi nilikuwa mgonjwa, na kwa baraka ya mchango mimi hali yangu sasa hivi ni nzuri zaidi, mimi sasa hivi nimeacha hata kutumia vodonge vya usingizi, nahisi utulivu katika moyo wangu. Baada yake akapata mvuto mkubwa kwa Allah, akatoa michango na kupata hamu ya ibada, na Allah akamjaalia fadhila nyingi, ambapo hapo nyuma hali yake ilikuwa mbaya sana kiasi cha kutaka kujiua.

Kuna rafiki mmoja kutoka U.K. anasema, hapo nyuma kwa muda fulani nilikumbushwa katika simu kutoa mchango wa Tahrik Jadid, na nikaambiwa kuwa mwaka uliopita nilitoa kiasi fulani cha mchango. Nami nilikuwa nimefanya ahadi ya kutoa mchango wa mwaka huu uliozidi kiasi hicho. Kipindi hicho mimi sikuwa na kiasi chochote cha pesa. Mimi nikaanza kumuomba Allah kuwa afanye mpango wa kupatikana fedha mahala popote kwa ajili hii, hivyo anasema baada ya wiki mbili nilipata ujumbe kutoka kitengo cha kodi, mimi nilikuwa nimezidisha kutoa kodi katika mwaka huo mzima nao walikuwa wanarudisha kwangu kiasi hiki kilichozidi. Mimi mwenyewe ni mhasibu nami ninajua fika hesabu ya kodi yangu vizuri, lakini Allah kwa muujiza mkubwa akaandaa mpango huu wa fedha kwa sababu sawa na hesabu yangu nilikuwa nimelipa kodi sawa sawa. Anasema baada ya muda mchache raisi wa tawi akanipigia simu tena na kunikumbusha juu ya mchango wa Waqf Jadid na akanijulisha kuwa mimi nimetoa mchango kiasi gani mwaka jana. Nami nilikuwa nimeandikisha ahadi yangu ya sasa kiasi kilichozidi kile cha mwaka jana. Kwa bahati mbaya wakati ule pia sikuwa na pesa yo yote. Nikaanza kufikiria kuwa Allah toka mwanzo alifanya mpango wa kurudi kwa kiasi kile cha kodi, sasa hivi hakuna sura nyingine yoyote ya kupata pesa. Anasema nikaanza kuomba dua, baada ya mwezi mmoja mimi nilikuwa napitia makaratasi yangu nikaiona bili fulani, ambayo ndani yake kulikuwa na ofa pia. Nikawapigia simu watu wa kampuni ile basi sawa na ofa ile wakanitengenezea kadi ya malipo ndani yake kulikuwa na kiasi cha pesa kilichozidi mchango wangu niliotakiwa kutoa. Hivi ndivyo Allah alivyofanya mpango wa kupatikana fedha za kutoa mchango wa Waqf Jadid. Sio kwamba hali hii Allah anaionesha katika Afrika pekee, bali katika kila sehemu. Kwani yule anayetaka kutoa mchango wake kwa nia safi lazima Atamuonesha matukio kama haya.....

# Bustani ya Washairi

**KIPI NILOTANGULIZA**

1. Sabauna sanatani, namshukuru Muweza
Ila swali la moyoni, kipi nilotanguliza
Barazani mwa Manani, ili nepuke gereza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

2. Nakuuliza mwenzangu, kipi tulichotimiza
Nafsi yangu ya tangu, toka nilipochomoza
Nieleze lile fungu, tuweke kwenye baraza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

3. Kipi unachokumbuka, kile tulotanguliza
Ahadi tuliposhika, tukaweza itimiza
Nipe nimeghafilika, tukumbushe tukiweza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

4. Ni wangapi masikini, wale wasiojiweza
Tulowapa afueni, njaa yao kupunguza
Ni wapi pia ni lini, heri tuliposambaza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

5. Walo kuwa utumwani, ukicha waomboleza
Makombo ya jalalani, ndio mlo wanameza
Sisi tulifanya nini, maovu kuyakataza?
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

6. Waliokabwa na kiu, ni vigumu kueleza
Ukaweza angalau, kwa sauti kutangaza
Ni vipi tumesahau, kiu inawaumiza?
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

7. Lengo letu la maisha, kumuabudu Muweza
Vipi tumekamilisha, Rabana aloagiza
Ni kwetu tulidumisha, ibada kutekeleza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

8. Kesho iwe kinga yangu, kipi nilotanguliza
Roho inayo machungu, sina nilichowekeza
Ninachoona ukungu, ni bahari yenye giza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

9. Rabi lino nahitaji, matendo ya muangaza
Huo kabiri mtaji, kuondoa kuteleza
Kwako Mola nataraji, utimie muujiza
Kipi nilotanguliza, kesho iwe kinga yangu?

**Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)**
Kiwalani – Migombani, Dar es salaam.

**UJAJI WA MASIHI**

1. Sifa zake mwenye shani, Mola twamuhimidia
Yeye ametuthamini, baraka katuletea
Twamshukuru manani, Mirza katuumbia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

2. Kashafika duniani, yeye tulimngojea
Kwa fadhila na hisani, Ghulamu kumtambua
Kuwa mtu wa thamani, yake kuyafatilia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

3. Kasimama ardhini, umoja katuwekea
Kila kona duniani, pembe zote za dunia
Watakuwa mashakani, wale wasomtambua
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

4. Ameamrisha dini, yake ya Mola Jalia
Uimara vitabuni, amekwisha fafanua
Katuwekea amani, tusijepotea njia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

5. Neno lake lifateni, mbele msijejutia
Pekueni vitabuni, ukweli mtagundua
Kashafika si utani, kuwa wa kufuatilia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

6. Alianza Nurudini, baraka alichukua
Walifika hamsini, kwenye kundi hadi mia
Hadi sasa milioni, idadi yaendelea
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

7. Allah ndio msukani, analotaka amua,
Mohamadi mfateni, elekea yake njia
Wa kukutoa gizani, ni Masihi ndio taa
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

8. Mwanga huu wenye shani, usiopoteza njia
Sofifia duniani, nuru yake sambazia
Utakuwa hatarini, kamwe sipokuwakia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

9. Maneno yenye kifani, yake alotugawia,
Funzo bora shika dini, sala tano ndio njia
Nguzo zote jipakeni, shetani kumuondoa
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

10. Michango msikitini, uwe mwenye wa kutoa
Wapendeni majirani, kuwa wa kusaidia,
Sadaka kwa masikini, Fungu lao jiwekea
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

11. Siingie kaburini, silo jambo la sawia
Na subira ishikeni, msiba kikufikia
Majivuno yaacheni, hayo ametuambia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

12. Nimefika ukingoni, hapa ninamalizia
Wale mlioamini, kamba moja shikilia
Maombi ndio rubani, pazuri kupafikia
Yeye tulimngojea, kashafika duniani

**Rehema Fadhili**
KITONGA DAR ES SALAAM

**KAMBA YA MASIHI**

1. Sauti sikilizeni, ya masihi muizani
Alotumwa na manani, aje kuhuwisha dini
Waliitupa thamani, waumini wa thamani
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

2. Elimu yake thamani, ituponye moyoni
Maradhi haya jamani, yasitubaki mwilini
Na tuyatowe moyoni, tuisafishe imani
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

3. Vitabu vyake makini, elimu yake indani
Tuvisomeni jamani, elimukae kichwani
Kungine tusitamani, tubaki humu ndani
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

4. Ndugu zangu jamani, masihi mpokeani
Umoja wake thamani, ndiyo njia ya mbinguni
Tuishike kwa makini, itufikishe mbinguni
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

5. Walomfaa masihi, mwenyezi kawa thamani
Wamishika kamba hii, ya muumba wa mbinguni
Masihi ndiye kiini, cha kufikia mbinguni
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

6. Enyi mlo pembeni, masihi mpokeani
Ni mjunbe wa manani, alotuwa duniani
Someni na koroani, ata ile imondani
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

7. Msimpinge tuyani,ushahidi umondani
Yule alompinzani, koroani yabaini
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

8. Kumbukeni wa zamani, walimtusi vikali
Umuongo wa shetani, unajifanya mkweli
Sisi hatukuamini, hata ukiwa mkweli
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

9. Masihi muhisani, akamuomba jalali
Nipe waja waumini, wenye kukubali ukweli
Waje kwako waumini, uwape njema amali
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

10. Jumuiya ya thamani, waungwana fahamuni
Dini gani duniani, yenye kamba ya thamani
Hakika sina utani, mbele ya mungu manani
Nasitusiikatani, ndiyo njia ya mbinguni

**Madumula Ng'amilo,**
**Tuangoma, Dar es salaam**

**AMANI**

1. Nyoyo zimefarijika, ukweli tumebaini,
Tumepewa mamlaka, na mola wetu manani,
Tutimize kwa hakika, Serikali wanadini,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

2. Ni tunu yake Rabuka, katufanyia hisani,
Tusiishi kwa mashaka, hii ni yetu thamani,
Tusije kudhalilika, tukiikosa amani,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

3. Amani kwetu Baraka, ikisitawi nchini,
Uchumi utaboreka, mjini na vijijini,
Tutazidi nawirika, kwa pamoja tutawini,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

4. Siasa hasi epuka, hatuutaki udini,
Na ukabila ondoka, hatupendi humu ndani,
Ndivyo tulivyoumbika, ili kulinda amani,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

5. Tanzania kwa hakika, ni kisiwa cha amani,
Kioo cha Afrika, na kwengine duniani,
Chunga kisije pasuka, tuingie matatani,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

6. Ukarimu twasifika, kila kona duniani,
Kwa utu twatambulika, twawajali majirani,
Hata tukose masika, hatumnyimi mgeni,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

7. Umoja tumeushika, japo tuna nyingi dini,
Abudu unachotaka, kile unachoamini,
Msikiti ukitaka, au nenda kanisani .
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

8. Makabila kwa hakika, haya kwetu burudani,
Kwa pamoja tunacheka, twataniana utani-,
Kiswahili chatumika, kila kona mikoani,
Tulinde yetu amani, isije ikatoweka.

9. Beti zimemalizika, kalamu naweka chini,
Sisi wote wahusika, lazima tuwe makini,
Na tumuombe rabuka, aidumishe amani,
Tilinde yetu amani, isije ikatoweka.

**Mwl. Najat Fakim Said Nangolo -** THE BIG BOSS
Ahmadiyya- Pawaga- Magozi- Iringa

**RABI TAKABALI DUA**

1. Yaillahi ya Satari, Mola Illahi Karima
Wewe ndi Msitiri, Mambo yote yaso mema
Ni hifadhi ya Kahari, Kwani dunia si njema
Rabi Takabali dua, Niachane na dunia

2. Hii dunia safari, Yawataka watu wema
Yale mambo ya ushari, Niyapitie kwa wima
Nakaa na kufikiri, Mola mwingi wa Rehema
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

3. Niepushe na kiburi, Mola mwenye sifa njema
Mie kiumbe hakiri, Naomba yako huruma
Nategemea shauri, hatima kwako Karima
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

4. Na kiburi kina shari, Hufuta zote neema
Maisha huwa shubiri, kuupunguza uzima
Na hivyo ndiyo hatari, Zigo kubwa la zahama
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

5. Nikinge na ufakiri, Nipande wako mlima
Bila ya wewe kahari, Napata wapi uzima
Na mafunzo yabashiri, Yakae kwenye mtima
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

6. Nizidi kuhubiri, Dini ya Mola Karima
Tena wingi uhodari, Kona za dunia nzima
Niwatie kwenye nuri, Islamu dini njema
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

7. Uniepushe na nari, Siku hiyo ya Kiama
Nitii zako amri, Bila moyo kutitima
Mchana Alifajiri, Si hofu yangu hatima
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

8. Najikinga kwa Ghafiri, Mola wangu taadhima
Dua yangu Nakariri, Rabi Mwingi wa neema
Sina mwingine wa siri, Nalia kwako Rahima
Rabi takabali dua, Niachane na dunia

**Rajabu Abasi Mkieti -** (Al-Wattan Mlezi)
Ikwiriri, Rufiji

**Dawa Ile Dawa Gani, Itulizayo Mtima?**

1. Bismillahi awali, nianze kwa kuchechema
Tungo ziwe bulibuli, nipate majibu mema
Anilinde na muhali, nisiipate lawama
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

2. Dawa ile dawa gani, itulizayo mtima
Nauliza wajamani, mtima unazozoma
Nipate na afuweni, akhera kawe salama
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

3. Dawa nimezijaribu, kwa idadi nyingi sana.
Mtima wanisulubu, nafuu sijaiona.
Dawa ipi matulubu, mwenzenu nipate pona
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

4. Walisema kitunguu, jitihada nilifanya
Ingawa siyo kichungu, harufu inakolanya
Mtima ungali juu, keroze zanichanganya
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

5. Dalasini niliwaza, dawa bandika bandua
Sikupata mazigaza, kwa ladha kunichefua
Mtima sijaupoza, wazidi kunitibua
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

6. Sijabakisha mzizi, siwezi yote kusema
Hata nayo tangawizi, sikuibakiza nyuma
Lo! Mtima wakaza uzi, ipi tanipa salama?
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

7. Nilichemsha majani, hata na mdimu pori
Uchungu kama kwinini, lakini nikahiyari
Nikomeshe kisirani, mtima sitakabari
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

8. Msidhani nalalama, ukweli ninaumia
Bila kupoza mtima, sitoipiga hatua
Yailahi ya Karima, Mola nisikize dua
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

9. Dunia hii mapito, kwa Allah marejeleo
Najikinga na majuto, mtima ukome leo
Mtima sipate moto, nataka maendeleo
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

10. Nautamani utoto, utumwa uso kemeo
Mtima tuliza joto, Allah nimuelekeo
Nikayapate mapato, akhera kuna vileo
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

11. Mtima lini tatubu, nipate matarajio?
Mtima punguza ghubu, Allah tanivesha nguo
Punguza na majaribu, nikipate kipozeo
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

12. Nitafanya sikukuu, dawa ile kiipata
Siyataki ya makuu, mtima wanicharata
Yailahi ya karimu, mja nipate takata
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

13. Wa akheri daawana, sifa ni zake Rabana
Akipenda Maulana, mtima tatulizana
Nipige na mbio sana, nifike mutumaina
Dawa ile dawa gani, Itulizayo mtima?

**Yusuf M. Juma** - (Sauti ya Nyika)
Dar es salaam

Kumkumbuka Rabuka, ni dawa mjarabati
Kunaondoa Shabuka, majuto na tashtiti
Maradhi yote hutoka, ukimpata Izati
Kuupata utulivu, mdhukuru Mola wako

***Mhariri***

# Mfalme na Viatu



Hapo zamani, palikuwa na Mfalme aliyeitawala nchi moja tajiri. Siku moja Mfalme alienda safarini kuelekea sehemu za mbali za nchi yake. Aliporudi kwenye kasri yake, alilalamika ya kwamba miguu yake inauma kwa uchungu sana, kwa sababu ilikuwa ni mara yake ya kwanza alikwenda safari ndefu kiasi hicho. Na barabara aliyotumia pia ilikuwa ina mawe sana na isiyochongwa.



Mfalme alidhania ya kwamba amepata wazo mujarabu sana. Aliwaagiza wafanyakazi wake kuitanda kila barabara katika nchi nzima kwa ngozi.

Kwa hakika, jambo hili lingehitaji mamia kwa maelfu ya mita za ngozi za ng'ombe. Bila shaka lingegharimu kiasi kikubwa sana cha rasilimali fedha.

Basi mmoja wa wafanyakazi wake wenye busara sana akadiriki kumuuliza Mfalme, "Kwa nini utumie kiasi chote hicho kisicho cha lazima cha fedha? Kwa nini usikate kipande kidogo tu cha ngozi ukafunikia miguu yako?"

Mfalme alishangazwa, lakini baada ya kulitafakari shauri lile, akakubali kufuata pendekezo la mfanyakazi wake, kutengeneza jozi ya 'viatu' kwa ajili yake.



Kuna somo kubwa sana katika hadithi hii: Ili kuboresha hali za imani yetu, ni bora kujibadili sisi wenyewe - tabia zetu, nyoyo zetu; na sio kutaka kuubadili ulimwengu wote. "....Hakika Allah Habadili yaliyoko kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nafsini mwao...." (Ar Ra'ad - 13:12)

# CHEMSHA BONGO



**KWENDA KULIA**
1. Nyumba ya Allah
3. Hali ya utulivu
4. Mwana mkuu wa Ibrahim
6. Mahubiri
7. Mwanzo
9. Wahandisi wa Kiahmadiyya
10. Utamaduni tangu na tangu
11. Kundi
14. Mashauriano
16. Nguzo ya tano ya Islam
18. Mwongozo kwa wanadamu
19. Kujitahidi katika njia ya Allah
21. Mmoja asiyefuatiwa au kutanguliwa
22. Shuka mbili
23. Nguo ya kuhifadhia maiti

**KWENDA CHINI**
2. Ibada kuu
5. Watoto wa kiume
8. Kiungo cha pilau
12. Tindikali
13. Watumishi
15. Uelewa/Fahamu/ Maarifa
17. Kukubaliana na sera/imani fulani
20. Unachoaminiwa kukitunza

**Majibu ya Chemsha Bongo la Toleo la Januari:** *Hongereni mliopatia yote*

1. MASROOR
1. MAKKA
2. RABWAH
3. NASAHA
4. MUHAMMAD
5. SALAAM
6. ADHANA
7. HIJA
8. RAKAA
9. IMAMU
10. RAMADHANI
11. AAM
12. NIA
13. KALAM
14. RAJAB

# TAFUTA MANENO

Yatafute maneno yafuatayo kwa kuyazungushia na Penseli

| | | | |
|---|---|---|---|
| DHARA | NUZUUL | TAJWID | RUZUKU |
| RAHIIM | KHAIBAR | MAKHZAN | TAKRIBAN |
| KAULI | MUSLIH | CHANDA | JAMIA |
| IHSAN | NAHNU | LANGAR | MHARIRI |
| DUTU | SHAHADA | MUSTAHABA | SHABABI |
| NJIA | TILAWAT | HAMASA | BISHARA |

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | L | N | I | H | A | M | A | S | A | Y | E | A | H | T | I |
| D | I | W | U | A | S | F | Q | A | X | C | Y | A | K | A | R |
| K | W | X | M | Z | D | H | B | R | C | J | R | L | J | K | Q |
| K | F | J | Y | I | U | A | A | U | K | A | P | K | L | R | P |
| N | Y | R | W | H | J | U | T | B | H | Y | B | R | A | I | T |
| T | N | J | U | A | C | U | L | D | A | X | X | M | N | B | I |
| W | A | S | T | Z | D | H | K | N | A | B | N | V | G | A | L |
| T | K | S | H | R | U | T | A | R | P | T | I | N | A | N | A |
| N | U | A | B | A | F | K | A | N | Y | K | R | M | R | M | W |
| M | B | L | U | W | H | H | U | H | D | H | Z | Y | T | G | A |
| Y | I | H | J | L | S | A | I | J | R | A | H | I | I | M | T |
| N | H | V | H | I | I | L | D | W | V | I | K | N | J | I | A |
| V | S | R | B | M | S | L | W | A | C | B | V | R | Q | J | V |
| N | A | V | A | U | M | A | K | H | Z | A | N | Q | M | N | L |
| R | N | J | M | T | N | A | H | N | U | R | R | T | X | B | X |
| N | M | X | R | W | N | P | M | H | A | R | I | R | I | R | X |

# Kambi za Malezi na Ijtimaa za Mikoa Zarindima

Na **Mwandishi Wetu**

Alhamdulillah, tunamshukuru Allah Muumba wa mbingu na ardhi, Aliyetujaalia afya na nguvu ya kutekeleza majukumu yetu sisi kama viumbe. Kwani Allah Anasema katika Qur'an Tukufu kwamba; "*Sikuwaumba majini na watu ila waniabudu*".

Kwa kuzingatia hayo Tanzimu ya Khuddamul Ahmadiyya imefanikiwa kuandaa kambi za Malezi na Ijtimaa za Mikoa takribani nchi nzima. Mikoa iliyoshiriki ni pamoja na Kagera, Geita, Simiyu, Shinyanga, Mwanza, Tabora, Dodoma, Morogoro, Mbeya, Iringa, Lindi, Mtwara, Pwani na Dar es salaam pamoja na Zanzibar. Jumla ya washiriki 806 walihudhuria. Kati ya hao Khuddam ni 437 na Atfal ni 369.


Geita


Mtwara

Katika kambi hizo wameshiriki wanafunzi na wasiokuwa wanafunzi. Lengo likiwa kukumbushana wajibu wetu na kujifunza mambo mbalimbali ya dini yetu tukufu ya Islam. Utaratibu huu ulianza takribani miaka 3 iliyopita, mwanzoni hatukuweza kufanya nchi nzima kutokana na mipangilio, lakini kwa msaada wa Allah mwaka huu tumeweza kushiriki nchi nzima na mafanimio yamekuwa makubwa sana. Alhamdulillah.

Katika Ijtimaa hizo yaliandaliwa mashindano ya kielimu na michezo mbalimbali. Mashindano ya kielimu yalikuwa ni Usomaji wa Qur'an Tukufu Tilawati, Uhifadhi wa Qur'an Tukufu, Kuhifadhi Sala ya Kiislamu, Kuhifadhi Hadithi 40 za Mtume (saw), Hadithi kutoka *Kiunga cha Watu Wema*, pamoja na mashairi. Lengo la mashindano haya ni kujipima kwa wanatanzimu kiwango chetu cha uelewa wa masuala ya dini yetu. Katika mashindano hayo washindi wa kwanza hadi wa tatu walipatiwa zawadi kama motisha. Lengo la kutoa zaawadi ni kuwafanya washiriki waweze kuongeza juhudi katika kufuatilia masuala ya dini na wale waliokosa wafanye juhudi ili katika Ijtimaa zijazo nao wafanye vizuri.

Pia Khuddam walishiriki michezo mbalimbali kama vile; mpira wa miguu, riadha, kurusha mkuki na tufe, kuvuta kamba, kuruka juu na chini na kuokota vikombe. Mashindano yanafanywa ili kuwaweka Khuddam katika hali ya ukakamavu na uimara wa afya. Katika kambi hizo sio kujifunza masuala ya dini na michezo tu bali pia paliandaliwa mpango wa kujitolea damu pamoja na kufanya usafi sehemu mbalimbali za kijamii. Alhamdulillah zoezi hilo lilifanyika na kuzaa matunda makubwa kwani limeacha athari kubwa katika jamii husika na kuitangaza Jumuiyya ya Ahmadiyya kikamilifu.

Sambamba na matukio hayo kuna tukio moja la kusisimua lililotokea huko mkoani Mbeya. Wakati Khuddam wamepeleka barua katika kitengo cha Damu Salama kanda ya Mbeya kuomba kujitolea damu na wakaruhusiwa, siku husika kitengo cha Damu Salama walienda Kanisani kuhamasisha waumini wajitolee damu ili kuokoa maisha ya ndugu zetu watanzania wanaofika Hospitalini wakihitaji damu. Lakini kwa bahati mbaya waliweza kupata unit 2 tu za damu, licha ya kwamba ilikuwa ni siku ya ibada ya jumapili wakielekea katika siku kuu ya Chrismas. Khuddam walijikusanya na kwenda wenyewe kutoa damu salama. Walikuwa Khuddam 15 pamoja na Ansarullah 2. Jumla ya chupa 10 za damu zilipatikana. Hata hivyo baadhi ya Khuddam wapatao 7 walikosa kuchangia kwa kukosa sifa stahiki. Baadae waumini walipotoka Kanisani walirejea kituo cha Damu Salama na kukuta Khuddam wamechangia chupa 10. Walishangaa sana kwa tukio hilo wakisema licha ya kwenda kuhamasisha watu wachangie damu, lakini wapo watu ambao wenyewe wapo tayari kuchangia damu kwa hiyari yao tena wanaleta barua rasmi kuomba ruhusa ya kuchangia damu. Hapo Qaid wetu wa Ilaqa- Mbeya aliwaambia kwamba utaratibu huu wa kuchangia damu katika taasisi yetu sio hapa Mbeya tu bali ni mpango wa nchi nzima.

Kwa kuthibitisha hilo mjumbe mmoja ambae alitokea mkoa wa Dar es salaam alionesha kadi yake ya uanachama na walipoona mfululizo wa tarehe za kuchangia walifurahi sana na kushukuru na kuahidi kufikisha ujumbe huu kwa Meneja wa kitengo cha Damu Salama Kanda ya Mbeya.

Hapa tunapata fundisho kwamba licha ya kuwa wachache lakini jambo tulilofanya limekuwa kubwa sana kupita la watu wengi. Hii ina maana kwamba wingi sio sababu bali kinachotakiwa ni imani. Katika dini Tukufu ya Islam tunafundishwa kuwa unapookoa uhai wa nafsi moja tu ni sawa na kuokoa umma mzima.

Katika kambi hizo Sadr Sahib aliweza kushiriki baadhi ya mikoa na mikoa mingine aliweza kuwateua wajumbe wake wa kumuwakilisha. Jambo hili pia lilizaa matunda makubwa kwani washiriki walifurahi kuwaona wajumbe toka Makao Makuu ambao waliwafikishia salamu na ujumbe toka kwa Sadr Majlis Majlis Khuddamul Ahmadiyya – Tanzania.

**Na neno letu la mwisho ni kuwa; Sifa zote njema zinamhusu Allah, Mola wa ulimwengu.**

# Mahafali ya Pili ya Khuddam Yafana

Na **Mwandishi Wetu**

Kwa msaada wa Allah na Rehema Zake tarehe 01/01/2019 Majlis Khuddamul Ahmadiyya Tanzania ilifanikiwa kuendesha mahafali ya pili ya kuwaaga ndugu zao Khuddam ambao wametimiza umri wa miaka 40 na hivyo kwa mujibu wa katiba ya Majlis Khuddam wamelazimika kuhama kutoka Tanzim ya Khuddam na kuingia katika Tanzim ya Ansarullah. Mahafali hayo yalifanyika katika ukumbi mpya wa Masjid Salaam uliofunguliwa hivi karibuni jijini Dar es salaam.



Mahafali haya ni ya pili, ambapo mahafali ya kwanza yalifanyika tarehe 01/01/2018. Katika mahafali ya mwaka huu jumla ya Khuddam 18 waliagwa rasmi kutoka Tanzim ya Khuddam na kuingia kwenye Tanzim yao ya mwisho ambayo watadumu nayo hadi mwisho wa maisha yao.

Kati ya walioagwa mwaka huu walikuwepo Masheikh wetu wawili wa Jamaat ambao ni Sheikh Asif Mahmood Butt Sahib; yeye ni Sheikh wa Jamaat Mkoa wa Morogoro na wa pili ni Sheikh Basharat Rehman Butt Sahib ambaye anaitumikia Jamaat akiwa ni Meneja wa kiwanda cha Uchapaji cha Jumuiyya yetu kilichopo Temeke – Dar es salaam.

Waagwa wengine ni; Bw. Issa Hassan Bunga Sahib ambaye ameitumikia Tanzim ya Khuddam kwa moyo mkunjufu na kujituma sana. Hadi anahamia Tanzim ya Ansarullah alikuwa anaitumikia Tanzim ya Khuddam kama Naib Qaid Dila ya Temeke. Mwingine ni ndugu Fadhili Abdulrahman Mikila Sahib ambaye alikuwa Naib Sadr Kanda ya Kusini. Alhamdulillah katika kipindi chake tangu ateuliwe katika wadhifa huo ameitumikia Tanzim kwa moyo mmoja na weledi mkubwa na kumshauri Sadr Majlis katika masuala ya Kitanzim ili kuweza kufikia malengo tuliojiwekea kwa ajili ya maendeleo ya Jamaat yetu. Mwingine ni Mwalimu Yusuf Mwishehe Juma Sahib ambaye licha ya kuwa mtumishi wa Jamaat na kuwa na majukumu mengi, lakini haikumzuia Sadr sahib kumteua kuwa Naib Sadr Utawala na Fedha, nafasi ambayo ameitumikia vyema hadi anamaliza muda wake.

Kuna tukio la kuongeza imani ambalo linaambatana na uteuzi wa Mwalimu Yusuf Sahib katika wadhifa huo. Ni hivi kuwa mara baada ya uteuzi wake, Mwalimu Sahib aliupokea uteuzi huo kwa mikono miwili na moyo mkunjufu na kumshukuru Allah kwani sawa na simulizi yake aliwahi kuonyeshwa katika njozi zaidi ya miaka 15 iliyopita wakati akiwa bado ni mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya Msingi Mwere iliyopo Manispaa ya Morogoro, katika njozi yake alijiona anapewea maagizo ya kutekeleza kwenye kipande cha karatasi na kiongozi asiyemfahamu lakini akijitambulisha kwa jina la Ramadhani. Alipoamka usingizini aliitafakari mno njozi yake lakini katu hakupata majibu yoyote. Mwalimu Yusuf anasema kwamba njozi hiyo katu haikufutika kichwani mwake na kila siku aliendelea kuikumbuka kana kwamba ameiota jana tu. Hivyo mara alipopewa barua ya uteuzi wake na Sadr Majlis, anasema mara moja fikra nzito ikamjia kichwani kwamba hiyo ndiyo taawili ya njozi yake ya zamani. Na baada ya hapo alianza kutekeleza majukumu yake aliyopewa, alifanya kazi kwa kujitoa, alitekeleza majukumu ya Tanzim aliyopewa na Sadr Majlis usiku na mchana. Kwa kipindi chote cha utumishi wake kwenye wadhifa huo ameweza kumshauri Sadr Sahib na kumsaidia katika majukumu mbalimbali ya uongozi wa Tanzim kwa shabaha ya maendeleo ya Tanzim na Jamaat kwa ujumla. Wakati alipotimiza umri wa miaka 40 Mwalimu sahib akijiandaa na kujiunga na Tanzim ya Ansarullah aliweza kufanya maombi maalumu na kufunga siku 40 akimshukuru Allah kwa kumjaalia kuweza kutimiza umri huu lakini pia kumuomba Allah ili Amjaalie yale aliyoyafanya akiwa Khuddam aweze kuyatekeleza zaidi katika Majlis yake mpya ya Ansarullah. Hao ndio Khuddam wachache walioagwa ambao wameweza kuwawakilisha wengine wasioweza kuhudhuria mahafali hayo.

Mgeni rasmi kwenye mahafali hayo alikuwa ni Amir na Mbashiri Mkuu– Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry. Wageni wengine walikuwa ni pamoja na Naib Amir Sahib Utawala–Issa Mwakitalima sahib, Sheikh Sahib wa Mkoa wa Dar es salaam, Katibu Mkuu wa ziada–Sheikh Abdulrahman Ame sahib, Sadr Ansarullah na baadhi ya Ansarullah pia walihudhuria mahafali hayo. Nao baadhi ya Khuddam waliweza kushiriki na kushuhudia mwenendo mzima wa mahafali hayo.

Katika mahafali hayo vyeti na nishani maalum vilikabidhiwa kwa waagwa kama ukumbusho na Amir Jamaat.

Hatimaye Amir sahib alitoa nasaha fupi na pia akawashukuru Tanzimu ya Khuddamul Ahmadiyya kwa kuandaa tukio lile adhimu kish kuongoza maombi ya kimya kufunga mahafali hayo.

Alhamdu Lillahi Rabbil 'Alamiin.

بسم الله الرحمن الرحيم

## JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA TANZANIA -
## KALENDA YA MATUKIO KWA NUSU MWAKA JAN. - JUN. 2019

| MWEZI | MWAKA | TAREHE | TUKIO |
|---|---|---|---|
| JANUARI | 2019 | 11 – 18 | Ahadi mpya za Waqf-e-Jadid kwa mwaka 2019. |
| | | 25 | Mitihani kutoka Kitabu cha: **Ushindi wa Islam** |
| | | 25 – 31 | Siku maalum za makusanyo ya mchango wa kawaida. |
| FEBRUARI | 2019 | 01 – 08 | Siku maalum za kuwaalika wageni kwa mazungumzo katika Jamaat zote. Taarifa zitumwe Makao Makuu. |
| | | 20 | **Siku ya Mwana Aliyeahidiwa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii). |
| | | 22 – 24 | Siku maalum za kuwatembelea wagonjwa, mahospitalini na majumbani. Pia kuwatembelea mayatima, walemavu, na vikongwe (washiriki, Ansar, Khuddam na Lajna). |
| MACHI | 2019 | 01 – 10 | Siku maalum za kufanya vikao vya kujadiliana ajenda za Shura ya 2019 na kuchagua wajumbe. |
| | | 09 – 10 | Mahubiri Maalum kwa kila tawi. (Viongozi wote ni lazima washiriki). |
| | | 15 | Mahubiri ya tarehe 09 – 10 yatolewe maelezo yake mbele ya Wanajumuiya wote. |
| | | 23 | **Siku ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii). |
| | | 31 | Siku ya mwisho ya kutuma dondoo za Mushawara kutoka matawini kwa ajili ya Shura ya mwaka 2019. |
| APRILI | 2019 | 05 | Mitihani kutoka kitabu cha: **Safina ya Nuhu** |
| | | 12 – 19 | Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya mchango wa Tahrik Jadid na Waqfe Jadid. |
| | | 27 - 28 | **Shura ya Kitaifa Dar es Salaam – mwaka 2019.** |
| MEI | 2019 | 06 | **Kuanza kwa mfungo wa mwezi wa Ramadhan*** |
| | | 10 –17 | Siku maalum za kukusanya malimbikizo ya michango. (Hasa mchango wa kawaida). |
| | | 17 | Wajumbe wa Shura wayaeleze matawi yao maazimio ya Shura - 2019 |
| | | 27 | **Siku ya Ukhalifa.** (Juhudi zifanywe ili Mkutano ufanyike siku hii hii). |
| JUNI | 2019 | 05 | **Eid Ul Fitri*** |
| | | 01 – 16 | Siku maalum za kuhakikisha kwamba kila Mwanajumuiya amekamilisha Bajeti ya michango yake hasa wa kawaida/Wasia sawa na kiwango cha kila mwezi. Juhudi maalum zifanywe. |
| | | 14-16 | **Ijtimaa ya Khuddamul Ahmadiyya Kitaifa.** |
| | | 21-23 | **Ijtimaa na Shura ya Lajna Imaillah Kitaifa.** |

*Zingatia: Saumu ya Ramadhani, na Sikukuu zote mbili zinategemea kuandama kwa mwezi.

# Kumbukumbu ya Alhaj Hemed Neema

Na **Mwl. Yusufu Gesonko Nyaghuyi**.
Shinyanga Mjini.

Alhajj Magambo Hemedi Neema mtetezi wa wanyonge aliyesimama kidete kumtetea Mwl Julius Kambarage Nyerere katika ile kesi ya kuwakashifu viongozi wa siku hizo; ma-DC na ma-PC. Shjaa asiyehofia vitimbwi vya binadamu aliyefikisha ujumbe wa Masihi kwa kiongozi Mkuu wa Nchi na kumpatia kitabu cha hotuba za Khalifatul Masih wa III Hadhrat Mirza Nasir Ahmad*rh* alipotembelea Afrika "Africa Speaks". Mwanajamaat aliyejijengea utamaduni wa kusoma, kutoa mali yake kwa njia ya Allah, ameitikia wito ule ambao kila binadamu anatakiwa kuitikia Rabbaika! Kwa hakika sisi ni wa Allah na Kwake tutarejea.

Alhajj Neema alizaliwa 1927 huko Musoma na kupata elimu yake huko huko Musoma. Mara baada ya kumaliza kunyonya alipelekwa kwa Chifu Makongoro kwani mke wa Chifu Makongoro alikuwa bibi yake mdogo. Itakumbukwa Chifu Makongoro alikuwa rafiki wa Chifu Borito Nyerere. Ni katika mazingira hayo ndipo alipopata fursa ya kufahamiana na Julius Nyerere ambaye walikua na kucheza pamoja. Ukaribu wao uliendelea na Alhajj Neema alitueleza baadhi ya mambo yanayohusu Mwalimu Nyerere na Jamaat Ahmadiyya. Kila alipokuja Dar es salaam alifika Masjid Salaam na kukutana na Maulana Sheikh Muhammad Munawwar. Ni wakati huo alipokuwa anakuja msikitini alipotueleza aliyokuwa anaambiwa na Mwalimu Nyerere "Waahmadiyya wana elimu sana, nawaheshimu sana. Mara nyingi nilikuwa najadiliana na Kaluta. Kuna siku nilimwambia ukinishinda nitakuwa Muislam."

Al Haji Hemed Neema alijiunga na jumuiya mwaka wa 1970 mjini Kisumu alikokuwa amewapeleka wake wa chifu kwenye matibabu Kisumu msikiti wetu umetazamana na Kisumu boys akaanza kusoma vitabu vya jamaat kupitia posta alijiunga mbele ya marehemu Maulana Hafidh Sulaimani aliyekuwa Sheikh wa Kisumu, baadaye Sheikh huyu alihamishiwa Mwanza ambapo alikumbuka mwanajumuiya wake ambaye alikuwa na anuani yake ya Nyamuswa Bunda akaamua kuja kumtembelea na ndipo watu wengine wakajiunga akiwemo Mzee Rashid Chakwanza, Abdulrahman Romole wa Bukama Ikizu, na wengineo. Japo kabla ya hapo Abdallah Meghabe Sindoma miaka ya 1965 alijiunga na jamaat mjini Dar es salaam. Mzee Hemed alikuwa kama Sheikh wa Ahmadiyya Mkoa wa mara sababu alikuwa mtu aliyeifahamu vilivyo jamaat Ahmadiyya. Alihudhuria mikutano yetu ya Jalsa Salana mjini Dar es salaam, amesoma vitabu vingi vya jamaat kila kitabu kilipotoka alinunua, Mzee Hemed akiwa Ahmadiyya alikuwa kiunganishi kwa Rais Nyerere na Jamaat yeye aliufikisha ujumbe haswa alipojitolea kumtolea ushahidi wakati watu wengine wametishwa kufanya hivyo na Serikali ya Ukoloni. Na Mwl. Nyerere alishinda ile kesi. Soma Kitabu *Kesi ya Julius Kambarage Nyerere* cha Simon Ngh'waya utakuta jina lake Mzee Hemedi wa Nyamuswa Bunda. Hivyo kwa ujasiri huo Mwl. Nyerere alimuona Mzee Hemed kama ndugu yake aliyejitoa kwa ajili yake bila uoga wa kutishwa na wakoloni. Mzee alikuwa ana upendo wa hali ya juu sana na jamaat. Alijitolea nusu ya pesa iliyonunua uwanja wa msikiti wetu. Alipenda sana msikiti. Alifanya usafi na kupalilia miti yetu ya michungwa na kupanda miti mingine ya matunda. Alisomba mbolea na kuhakikisha kuwa miti inastawi. Nyumbani kwake palikuwa sehemu ya ibada kwa Waahmadiyya wa Nyamuswa. Kwenye michango alikuwa mstari wa mbele hususan michango ya Tahrik Jadid na Wakfu Jadid aliyokuwa akikamilisha ahadi yake kabla mwaka kuisha. Alikuwa Rais wa Tawi la Nyamuswa kwa muda mrefu sana mzee Sindoma akiwa katibu wake. Aliwahi kuhiji Makka. Mwalimu wa tawi alimshauri kumuandikia barua Khalifa mtukufu kwa ajili ya maombi juu ya watoto wake. Majibu yalikuja kwamba mmoja kati ya watoto hao atafanikiwa sana. Watoto waliweza kuijenga nyumba ilipoanguka na pia kuzijenga za kwao. Kwa hakika maombi ya Makhalifa wetu yanapokelewa haraka sana. Majibu tya barua hii imetunzwa hadi sasa kwa kumbukumbu.

Alhajj Magambo Hemedi Neema alifariki mwezo wa kumi mwaka 2018. Sisi sote ni wa Allah na Kwake tunarejea.

Mungu amlipe malipo mema huko akhera na aihifdhi familia yake ifuate nyayo zake Amiin.

**Afya ya Amir Jamaat yazidi kutengemaa**

Baada ya kufanyiwa matibabu katika hospitali ya Muhimbili na kuruhusiwa siku iliyofuata, afya ya Amir Jamaat imekuwa ikizidi kutengemaa na kupata fursa ya kuanza kurejea katika majukumu yake kidogo kidogo kwa kadri ya ushauri wa madaktari walivyoelekeza. Na kwa sasa ameweza kuongoza sala mbalimbali na vikao vya Majlis Amila kama kawaida. Ofisi ya Amir Jamaat inawashukuru wanajumuiya wote kwa maombi waliyoelekezwa kwa Amir Jamaat na maombi hayo yaendelee pia kwa wagonjwa wengine ili Allah afanye tahfifu na kuwaondolea maradhi yao. Amin.

# MATUKIO KATIKA PICHA



*Rais wa Kanda ya Ziwa akiwanasihi wanajamaat wakati wa ziara akiwa pamoja na Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat katika Kanda hiyo*



*Naib Amir Tabligh na Tarbiyyat akiwa na wanajamaat wakati wa ziara yake katika Kanda ya Ziwa*



*Naib Amir Tarbiyyat na Tabligh akiwa na wanajamaat wakati wa ziara ya Kanda ya Ziwa*




*Programu ya Mahubiri ya Vibanda ikiendelea stendi ya mabasi Mnazi Mmoja*



*Khuddamul Ahmadiyya wa Dar es salaam wakiwa katika operesheni ya usafi ya #TuitunzeMisikiti katika msikiti wa Masjid Salaam ilipo Makao Makuu*



*Washiriki wa Kambi ya Malezi na Ijtimaa ya Mkoa wa Dar es salaam na Pwani*



*Sheikh Musa bin Isa akimkabidhi Atfal zawadi ya ushindi katika Kambi ya Malezi na Ijtimaa ya Dar es salaam na Pwani*

# Lengo la Dini Sio Siasa au Kuwa na Dola

*Inatoka uk 1*

Nabii Isa bin Mariamu[as] (Yesu) hakupigana vita licha ya mateso makubwa kwa watu wake na yeye hata kuwekwa msalabani. Isa bin Mariamu[as] alikuwa Masih wa Musa[as], Musa[as] akipigana vita na Masih wake hakupigana.

Ndivyo ikawa kwa Mtume Muhammad[saw] ambapo alipata mateso kwa muda mrefu, inakadiriwa kuwa miaka 13 na ndipo alipoambiwa na Allah apigane vita. Umri wa Mtume[saw] wa utume wake ulikuwa miaka 23 tu. Kama ilivyokuwa kwa Nabii Musa[as] na masih wake ndivyo Mtume[saw] alisema Masihi wake atafuta vita vya upanga katika dini. Kwa amri hii Utume sharti uendelee ili afike Mtume atakayefuta vita ya upanga. Na yeyote anayemkataa Mtume huyu ataendeleza vita ya upanga kwa dhahiri au siri.

Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Hazrat Mirza Ghulam Ahmad[as] Masih Aliyeahidiwa na Imam Mahdi amekwisha fika. Mtu huyu aliyesubiriwa na dini zote keshafika na kufika kwake amefuta vita yeyote katika dini. Walio wapinzani wake imani hizi ya vita bado zimo mioyoni mwao. Waislamu wanauana wao kwa wao, Waislamu wakiwauwa wasio kuwa Waislamu na huku wakiwatesa na kuwauwa Ahmadiyya. Dini zingine kwa kuwa nao hawana muongozo wa kimbingu sasa wamekuwa wakijibu mapigo. Tumeshuhudia mapigano ya Wakristo na Waislamu nchini Nigeria, Mali, Asia n.k.

Islam ya Ahmadiyya imeendelea kuumizwa kwa kuharibiwa mali zake na viongozi wake kuuwawa na watu wake. Tumeshuhudia Pakistani ikikidhiri kwa dhuluma hii, Algeria, Indonesia na nchi nyingi walipo Waahmadiyya kwa kunyang'anywa wake, mali na kuuawa. Ni mwaka jana 2018 walibomoa msikiti wa historia wa jamaat, Masjid Mubaraka; mwaka 2010 walivamia misikiti yetu huko Pakistan na kuua watu wengi kabisa katika historia ya mauaji katika dini kwa miaka ya zama hizi. Ila haijawahi na hata kufikiriwa kujilipiza kisasi.

Dhana ya mauaji katika dini ni kwa sababu tu wenye dini wametaka kuchukua malengo ya dola na hivyo kila dini sasa inatetea imani yake hata kwa nguvu kwa sababu tu ya kumiliki dola na kuwa dini kama dola. Namna hii misingi ya asili ya dini hupotea na kuigeukia dunia. Sawa na aya hii niliyotangulia kuikariri ya 2:257 na nyingine za 18:30 na 10:109 zilitaka masuala ya dini yaachwe kuwa huru na hiyari ya mtu na yasihusiane na dola. Hata Mtume[saw] alipotawala na kuwa na dola alihukumu kwa sheria za Islamu kwa Waislamu tu na kuwaacha wasio kuwa Waislamu kuhukumiwa na sheria za dini yao. Sheria maarufu sana ya mzinifu kupigwa mawe mpaka kufa ni sheria iliyoamuriwa kutumika kwa mwanamke mzinifu wa kuyahudi ambao wao ndio huamini wa sheria hiyo. Hakuna kumbukumbu ya kihistoria kwa sheria ya Kiislam mzinifu kupigwa mawe. Uhuru na hiyari hii ya dini sawa na aya hizo umetaka yafuatayo.

1. Kuwa kujiunga na dini na au imani yeyote ya dini kuwe jambo la hiyari ya mtu na asiwepo mtu wa kumlazimisha au kumshurutisha, kumtesa, kujiunga na kumuwa ili kumlazimisha ajiunge.
2. Asiwepo mtu kuteswa, kufungwa, kushurutishwa (kwa hiyari au makusudi), na kuuwawa pindi atakapo iacha dini.
3. Dini isiwafunge, kuwatesa, kuwa shurutisha na au kuwauwa wale wote watakagoma kujiunga na dini yako.
4. Dini izingatie misingi ya haki ya binadamu. Hapa pia dini na dola inatofautiana juu ya misingi ya haki za binadamu. Dola misingi ya haki ya binadamu imestawi kwenye haki sawa, mipaka ya adhabu, kusameheme malipo. Wakati dini misingi ya haki za binadamu zimestawi juu ya uadilifu yaani, kuadhibu sawa na kosa, kusamehe na malipo. Kosa moja mfano: aliyeuwa kwa makusudi kwenye misingi ya dola asiuawe, ila Islamu ikitaka huyu aliyeuwa kwa makusudi auwawe na sio kila mmoja wake auwe hii sio maana yake ila dola ndio itekeleze.

Nchi hizi za asili dini itabaki katika ulinzi wake Allah. Allah anawatangazia kuwa atakayetaka kuzima nuru yake hataweza na ni lazima dini yake ishinde hata makafiri wachukie. Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya kwa kushika njia hii ya asili na licha ya kufungwa kwa watu wake, mateso inayoyapitia na kuyapata na mauaji yanayoendelea kwa jina la dini. Ndio taasisi pekee inayokuwa kwa kasi kuliko taasisi yeyote hapa duniani, ambapo imefika kwenye nchi 212 ambapo mtawanyo huu haupatikani kwingine popote. Ni Ahmadiyya ndio inayokuwa kiasi hiki Waislamu na Wakristo na wasio kuwa Waislamu kutishiwa uhai wa dini na imani zao.

Tunamuomba Allah Atujaalie kuwa Waislamu na Atujaze kheri, rehema na fadhili Zake ndani yetu. Amin

# Bishara ya Mwana Aliyeahidiwa na Majukumu Yetu

*Inatoka uk 12*

***Mwana wa ahadi atakuwa mdhihirishaji wa sifa za Allah Aliye wa Mwanzo na wa Mwisho.***

Katika maneno haya, imebainshwa ya kwamba Mwana Aliyeahidiwa atadhihirika na katika zama zake fitina nyingi dhidi ya umoja wa Jamati zitaibuka. Kwa sababu hii kutakuwa na changamoto nyingi za kifedha na za aina nyingine naye atawajibika kukabiliana nazo na kubakiwa na baadhi ya vitu vya msingi tu.



Sheikh Shahab Ahmad

Hadhrat Khalifa wa Pili, al Musleh-ul-Maud[ra] alianza kazi yake katika hali kama hii. Ikiwa mtu anakabidhiwa kazi yoyote katika hali tete anasita na kutia wasiwasi mwingi kabla ya kuipokea. Lakini dunia nzima ilishuhudia ukweli wa neno la Allah subhana wataala kutimia sawasawa kwamba Mwana Aliyeahidiwa kadri ya uwezo wake alipokea kwa moyo wote na akaendelea kutekeleza kazi yake kikamilifu mpaka kuimaliza. Hivyo ndivyo ilivyobainishwa katika bishara itokayo kwa Allah subhana wataala kwamba Mwana Aliyeahidiwa atakuwa mdhihirishaji wa sifa Zake.

Hakuna kazi yoyote aliyoiacha njiani bali akapumzika baada ya kuitekeleza na kuimaliza. Kazi alizoanzisha katika maisha yake tunashuhudia nyingi zao zimestawi na kuzaa matunda mpaka leo hii na INSHA'ALLAH vizazi vijavyo vitaendelea kujinufaisha na matunda hayo mazuri.

Sifa hii pia kila mwanajumuiya anatakiwa awe nayo. Mwahmadiyya kila akianza kazi, asichoke bila ya kuimaliza kwa kuitendea haki ipasavyo. Mola wetu Haridhiki kwa kufanya nusu kazi. Baadhi ya watu huanza kazi kwa shauku kubwa lakini njiani wanachoka. Kwa hiyo, kadri na uwezo wetu tunatakiwa kuendelea kuchangia katika maendeleo ya jumuiyya bila ya kuchoka. Mwana Aliyeahidiwa[ra] alisema katika ubeti wa shairi lake akitusihi:

*"Bila shaka kazi hii ya kusambaza ujumbe wa Allah duniani kote ni ngumu mno, mwisho pia ni mbali na yawezekana kupata matatizo na taabu njiani, lakini enyi wapenzi Waahmadiyya waaminifu, mnaodai kuwa na uhusiano na mimi, mnalazimika kutochoka asilani na kuendelea kusambaza ujumbe huu mpaka mwisho wa maisha hadi dunia nzima ing'ae na nuru ya Mola wake."*

**Bishara nyingine** ni kwamba:

*"**Mataifa yatabarikiwa kwa sababu yake.**"*

Sehemu hii ya bishara ilitimia sawasawa katika uhai wa Mwana huyo Mtukufu. Mbali na kudhihirisha ukweli wa Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] bishara hii inathibitisha kwamba Islamu ni dini ya watu wote na zama zote.

Katika zama za Mtume mtukufu[saw] mbegu ya dini Tukufu ya Islamu iliyopandwa, ilimea mzizi na mimea yake ikaenea mpaka nchi za Ulaya, Uajemi, Misri na Uhabeshi. Hatimaye, kwa baraka za mbegu ile, bustani nyingi zenye matunda mema ya Islamu zilistakimu duniani kote.

Muda ulivyoenda bustani hizi zikaanza kunyauka na hali ya Waislamu kuinama chini, kama ilivyotabiriwa na Mtume Mtukufu[saw]. Allah subhana wataala kwa kutimiza ahadi yake, Alituteremshia Masihi Aliyeahidiwa[as] na katika ufuasi wake Mwana Aliyeahidiwa aliyeendeleza misheni yake kwa kueneza mafundisho sahihi ya Islamu kwa ajili ya kaumu zote na mataifa yote ya dunia.

Katika enzi ya ukhalifa wa Hadhrat Musleh-i-Maud[ra], wabashiri wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiyya walianza kutumwa katika nchi mbalimbali kuuhubiri Uislamu, na matawi mapya ya Jumuiya yakaanza kupatikana katika karibu kila nchi iliyokukuwa tayari kupokea wabashiri wa Islam kufanya kazi yao. Mwana huyu wa ahadi alijulikana mpaka pembe za dunia na mataifa mengi yalibarikiwa kwa sababu yake.

Basi kutokana na sifa hiyo ya Mwana Aliyeahidiwa, jukumu muhimu la Waahmadiyya ni **kushiriki katika kazi hii nyeti ya kuyabariki mataifa yote ya dunia kwa kusambaa dunia nzima na kueneza mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islamu kwa watu wote ili waongoke na kumtambua Mola wao**. Tukishatekeleza majukumu yetu tutakuwa na stahiki ya kuonesha furaha yetu na kutoa shukrani zetu kwa Allah kwani ishara ya kimbinguni imetimia na shani yake kudhirika. Allah subhana wataala Atujaalie kukumbuka wajibu wetu kulingana na bishara hii na kuutekeleza kadri iwezakanavyo. Aamin

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

# Mapenzi ya Mungu

JAM. I-JAM. II 1439 AH | FEBRUARI 2019 | TABLIGH 1398 HS

**Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w**

Imesimuliwa na Hadhrat Abdullah bin Umar r.a. ya kwamba Mjumbe wa Allah s.a.w. alisema: Mbora miongoni mwa marafiki ni yule aliye mbora wao kwa mwenzake. Na jirani bora mbele ya Allah ndiye anayemtendea vizuri jirani yake. (Tirmidhi)

# Bishara ya Mwana Aliyeahidiwa na Majukumu yetu

Na Sheikh Shahab Ahmad
Dar es Salaam

Sisi waahmadiyya tunajua vizuri tarehe 20 Februari inatambulika kuwa ni siku ya Mwana Aliyeahidiwa na kuadhimisha kutangazwa kwa bishara hii adhimu. Katika siku hii Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] alifunuliwa kuhusiana na kuzaliwa kwa mwanaye atakayekuwa na sifa kemkemu. Bishara hii tukufu inaonesha adhama ya Mtume Mtukufu[saw] na vilevile ukweli wa Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] na inadhihirisha kuwa kwake kutoka kwa Allah subhana wataala.

Mwana huyu wa ahadi alikuwa Khalifa wa Pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as] ambaye ni Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad[ra] aliyeteuliwa kuwa Khalifa mnamo mwaka 1914, na baada ya kupata mwongozo utokao kwa Allah mwaka 1944 akatanga`za kwamba bishara ya Mwana Aliyeahidiwa inatimia barabara katika dhati yake.

Bishara hii ilitangazwa na Hadhrat Masih Aliyeahidiwa[as] mnamo mwaka 1886 ambapo aliondoka kwao Qadian na kwenda mji mwingine wa Panjab uitwao Hoshiar Pur ili kumwomba Allah subhana wataala Aonyeshe ishara ya kuisaidia Dini ya Islamu. Maombi yake kwa siku 40 mfululizo yalikubaliwa na ahadi ikawekwa ya kumtuma roho aliyebarikiwa ambaye atadhihirika na sifa zake tukufu zitaenea duniani kote. Ufunuo huo wa Mwana Aliyeahidiwa ni bishara iliyotolewa kama matokeo ya maombi yake.

Bishara hii inayoanza na maneno haya: ***NINAKUPA ISHARA YA REHEMA YANGU***, ina umuhimu mkubwa katika Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Hii ilikuwa ishara ya Qudra, uwezo, ukarimu na ukaribu na Allah, nayo ilikuwa ishara ya rehema na ihsani ya Allah. Katika ufunuo huo Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa[as] akapewa ufunguo wa ufaulu na ushindi. Kila atakayesoma maneno yake kwa kina, bila shaka, anaweza kuelewa vizuri shani ya bishara hiyo ya kipekee.

Bishara hii inazaa maswali muhimu kwamba je, bishara hii inamhusu mtu mmoja tu? Je, sisi Waahmadiyya tunatakiwa kuridhika na kukaa kimya kwa sababu katika dhati ya Hadhrat Khalifa Mtukufu wa Pili[ra] bishara au ishara hii adhimu ilitimia sawasawa? Je, bishara hii inatukumbusha majukumu yetu? Au kama tunatakiwa kutoa shukrani kwa Allah, je ni njia gani zinazofaa kumshukuru ipasavyo?

Tukiangalia kwa jicho la upekuzi, umuhimu wa bishara hii unazidi kudhihirika kwamba bishara hii haimhusu mtu mmoja tu, bali kwa kweli, inatujulisha kwamba ujumbe wa Hadhrat Masih Aliyeahidiwa[as] ni wa kimataifa nao utaenea duniani kote na utaendelea kudumu na kufaulu milele.



*Khalifa wa Pili wa Masihi Aliyeahidiwa[as]*
*Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad[ra]*

Ni ukweli usiopingika kwamba ikiwa Allah Anataja baadhi ya sifa za Imamu wa Jumuiya, bila shaka mradi wake ni huu kwamba wafuasi wa Imamu huyo pia wanatakiwa kushika rangi ya sifa hizi. Yatupasa kufahamu kwamba Imamu ni kama injini ya gari moshi na wafuasi wake kama mabehewa yanayoifuata. Mabehewa huunganishwa na injini ili iyaongoze kuelekea kituo sahihi. Behewa lo lote lisiloweza kuendana na kasi ya injini, litaachwa nyuma mpaka likarabatiwe na magurudumu yake yote yaendane vizuri na mwendo wa injini.

Allah subhana wataala alipotaja sifa za Mwana Aliyeahidiwa[ra] anamaanisha kwamba, waahmadiyya pia wanatakiwa washike sifa hizi katika nafsi zao ili wanufaike nazo. Hili ni jambo muhimu la kutafakari na ni kiini cha bishara hii. Sifa nne zifuatazo kutoka katika bishara hii zitaelezwa hapa kwa kifupi ili tujue zinatukumbusha nini.

**Sifa ya kwanza** ni hii:

Mwana wa ahadi *"**atawaponya wengi wenye maradhi kutokana na baraka za Roho ya kweli.**"*

Hii ni alama ya kila mteule wa Allah. Mwenyewe huwajaalia ukaribu naye nao kwa nafsi zao takatifu husafisha na kuwaponya wagonjwa wa kiroho. Kwa huruma waliyo nayo kwa binadamu, wanashauri watu vizuri kuhusu maradhi ya kiroho na kuwaambia njia mbalimbali ili yaondolewe mbali.

Kwa hakika alama hii ilithibitika katika dhati ya Hadhrat Mirza Bashir-ud-Din Mahmood Ahmad, Khalifa Mtukufu wa Pili[ra], na halikadhalika inatusisitiza kwamba tuwe na sifa hiyo ili kupata ukaribu na Allah. Kiwango cha kupata ukaribu na Allah ni neema kuu kati ya neema zake zisizohesabika. Waislamu wote wanahimizwa kuongeza katika imani yao na kuwa miongoni mwa watu waliotajwa katika aya hii ya Sura Haa Mim, isemayo:

*"Hakika wale wanaosema, Mola wetu ni Allah, kisha wakaendelea kwa kudumu, huwateremkia Malaika (wakiwaambia) msiogope wala msihuzunike, na ifurahieni Pepo mliyokuwa mkiahidiwa."*

Sisi Waahmadiyya ni wale wanaodai kuwa na mafundisho sahihi ya dini tukufu ya Islamu. Ndio wale waliopewa jukuma la kuwatahadharisha watu wapotevu na kuwaongoza katika njia sahihi ya imani. Tumeahidi kusambaza mafundisho haya katika jamii yote bila kujali tofauti ya kabila, rangi au taifa ili tuwakusanye watu wote chini ya Imamu mmoja wa zama, Hadhrat Khalifa tul Masih. Hatuna budi kuwa mfano mwema katika jamii ili watu wengine wapate kuiga mwenendo wetu mzuri. Kwa sababu tunaweza kumfaidisha mtu mwingine na kitu tulicho nacho tu. Hatuwezi kumwita mwingine kama tusipokuwa na chochote chenye faida kwake. Kwa hiyo ni lazima tuishike dawa hii ya ponyo kikamilifu yaani ukaribu na Mola wetu ili tuweze kuwaponya wengine na maradhi ya kiroho.

**Sifa ya pili** ya Mwana Aliyeahidiwa iliyobainishwa katika ufunuo utokao kwa Allah subhana wataala ni:

*"atajazwa elimu ya nje na ndani". Inamaanisha kuwa elimu ya kidhahiri na ya batini, au ya dunia na ya kidini."*

Sifa hii pia ni muhimu sana kwa kila kiongozi wa kiroho na vilevile inahitajika kwa waaminio waliopo katika ufuasi wake. Bila ya kupata kiasi fulani kutoka katika sifa hiyo, hakuna mtu anayeweza kuwaongoza wengine.

Hadhrat Khalifa Mtukufu wa Pili (al Musleh-ul-Ma'ud) alipata elimu za aina mbalimbali kutoka kwa Mola wake. Hususani elimu ya tafsiri na maelezo ya Quran Tukufu aliyopata, ilikuwa ya hali ya juu hata wanazuoni wa zama zake hawakuweza kushindana naye. Yeye mwenyewe anasema:

*"Mimi niliambiwa na Allah katika njozi ya kwamba nimepewa elimu ya Qurani Tukufu kutoka kwake, na pia ninawatangazieni tangu miaka ishirini na kadha, ya kwamba angekuwa mwana falsafa yeyote au professa wa dunia au mwanachuoni yeyote — hata aliyepata shahada kutoka Uingereza — au bingwa yeyote wa elimu yoyote, anayetoa dai lolote dhidi ya Qur'an au dini Tukufu ya Islam, mimi kwa fadhili za Allah nitamjibu kwa jawabu la kutosha. Hakuna elimu yoyote ya kidunia ambayo Allah hajanipatia vipengele vyake."*

Umuhimu wa kupata elimu ulisisitizwa sana na Mtume Mtukufu[saw] na tunaagizwa kwamba tupate elimu hata tungelazimika kupata taabu ya kusafiri mbali ni lazima twende, tukaitafute na kufaidika nayo. Hadhrat Muslih e Maud[ra] katika maisha yake yote alifanya bidii kutoa elimu na mafundisho aliyopata kutoka kwa Allah. Sasa tunavyo vitabu vyake vyenye mafundisho hayo vilivyotokana na bahari ya elimu yake isiyokuwa na mipaka. Kila mwanajumuiya analo jukumu la kusoma matoleo ya hotuba, maandiko na mashairi yake na vilevile kujiongezea elimu katika nyanja zote. Katika shairi lake moja alisema:

*"E mwenzangu, mbona umeridhika kukaa ukitulia sehemu moja? Mimi nimejaa hamu ya kumtumikia Allah nami ninatafuta moyo wenye shauku ya imani kama hii."*

**Sifa ya tatu**, inatokana na maneno haya katika bishara:

*Endelea uk. 11*